## ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

### MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh’d Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| **Ndugu Yahya Khamis Hamad** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi** |

**BARAZA LA WAWAKILISHI - ZANZIBAR**

**BARAZA LA NNE LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 13 Mei, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

## WIMBO WA TAIFA

*(Wimbo wa Taifa uliimbwa kuashiria kufunguliwa kwa Mkutano)*

## DUA

Mhe. Spika, *(Pandu Ameir Kificho)* alisoma dua

## TAARIFA YA SPIKA

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, karibuni sana katika mkutano wetu wa ishirini Baraza la nane, Baraza ambalo ni maalum kwa shughuli za bajeti na kama kawaida kila kunapokuwa na shughuli ya kazi nzuri mliyofanya nyinyi huwa tunatoa taarifa ya Spika.

Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa Kumi na Nane wa Baraza la Nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 21 Januari, 2015 hadi tarehe 30 Januari, 2015. Baraza limepitisha Miswada minne ya Sheria ambayo ni kama ifutavyo:

Kwanza Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Sheria ya Kupunguza na kukabiliana na maafa Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada wa Pili ulikuwa ni Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada wa Tatu ulikuwa ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu namba mbili ya mwaka 1996 na kuweka badala yake Masharti bora ya uhifadhi kulinda na kusimamia mazingira Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada wa Mwisho wa nne ni Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kati ya Miswada hiyo minne, Miswada mitatu ambayo ni Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya kupunguza na kukabiliana na maafa Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo, na Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo, na Mswada mwengine wa Tatu ni Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo endelevu namba mbili ya mwaka 1996. Na kuweka badala yake masharti bora ya kuhifadhi kulinda na kusimamia mazingira Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 61 kifungu kidogo cha tatu cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012.

Naomba kutoa taarifa kwenu Waheshimiwa Wajumbe kwamba Miswada hiyo mitatu sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kwa kupokea taarifa hiyo, tunaendelea.

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwanza kabisa tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tena kukutana katika Baraza lako hili tukufu, baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 1 Aprili,2015.

Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: M**he. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya hali ya uchumi kwa mwaka 2014 na Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2015/2016.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha hotuba ya kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2015/2016. Naomba kuwasilisha.

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 17

### Kumalizia Ujenzi wa Jengo Jipya la Chuo cha Mafunzo Kengeja

**Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) -** Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwanza nashukuru kupata nafasi hii na kwa niaba ya Mhe. Mwakilishi naomba swali lake Nam. 17 lijibiwe.

Kwa kuwa Kambi ya Chuo cha Mafunzo yenye wanafunzi tisa kwa sasa, iliyoko Kengeja ni miongoni mwa vyuo vya mafunzo vya SMZ. Na kwa kuwa majengo yote yaliyoko katika chuo hicho ni mabovu, yaliyokosa kiwango na yasiyostahiki kuwekwa mahabusu wala Askari kutokana na uchakavu mkubwa uliopo katika majengo hayo.

Je, ni lini Serikali itamalizia kujenga lile jengo moja lililoanza kujengwa kwa juhudi za askari wetu pamoja na kujenga angalau jengo moja la Utawala.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Chuo cha Mafunzo kimejenga jengo jipya Kengeja ambalo limefikia hatua ya kuezekwa, na kwa sasa hatua iliyobakia ni kuweka milango, madirisha, kupigwa plasta na kuwekwa *"fitting*" ya umeme. Baada ya kumalizika jengo hilo, Chuo cha Mafunzo kitaanza ujenzi wa jengo la Utawala pamoja na nyumba za kuishi askari.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ya kuelekeza kujenga jengo jengine baada ya hili, mimi ningeomba nijibiwe swali langu kama ifuatavyo. Kwa sababu jengo ni la zamani na limechukua muda mrefu mpaka ikabidi kuletwa suala hili hapa Barazani. Je, kwa nini jengo hili likachukua muda mrefu mpaka leo ikawa halijamalizika na baada ya kumalizika, lina uwezo wa kuchukua wanafunzi hawa tisa tu au kuna mipango mengine. Na je, ni kiasi gani ya gharama zitumike hivi sasa mpaka kumaliza kazi iliyobakia.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, jengo tunalolijenga si la zamani ni jengo jipya, isipokuwa jengo

lilovunjika na tukaanza mpango wa kujenga jengo jipya hilo lilikuwa la zamani. Kwa hiyo, baada ya kwisha kuvunjika jengo la zamani ndio tukawahamisha wanafunzi tukawapeleka Wete na tumeanzisha jengo jipya ambalo litagharimu milioni 40 mpaka kukamilika kwake na mpaka sasa hivi limeshatumia milioni 19.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, nilikuwa nataka kumuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha jengo jipya na la kisasa na lenye hadhi ya kujali haki za binadamu katika eneo la Hanyengwamchana ili kuwawekea mazingira mazuri wale watu ambao wanahukumiwa au kufungwa au kufungwa katika magereza yetu.

Je, Serikali ina mipango gani ya kuanzisha ujenzi wa jengo jipya la Magereza kama lile ambalo limeanza kujengwa Hanyegwamchana kwa upande wa Pemba?

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Ni kweli Serikali imeandaa mpango wa ujenzi wa jengo jipya la Magereza katika eneo la Hanyegwamchana, bado Serikali inaendelea na kujenga ukuta wa jengo hilo na kwa sababu jengo hilo litagharimu pesa nyingi Serikali bado inatafuta namna ya kuweza kupata wahisani na washirika wa Maendeleo na kutenga bajeti yake yenyewe pale muda muafaka utakapofika ili jengo hilo liweze kujengwa katika eneo la Hanyegwamchana. Baada ya kumalizika kwa ujenzi huo wa jengo jipya la Hanyegwamchana, Serikali vile vile itaandaa mpango madhubuti wa kutengeneza mradi wa kujenga gereza jipya katika kisiwa cha pili cha Pemba.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri suala moja la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwa kuwa suala la msingi ilikuwa ni kuhusu ujenzi wa jengo la Kambi ya Kengeja na kwa kuwa Jengo lile halijakamilika, sasa naomba nimuulize Mhe. Waziri, jengo lile linatarajiwa kukamilika lini, hilo ni (a)

Lakini (b) ni hatua gani za dharura ambazo Mhe. Waziri anakusudia kuzichukua ili kuhakikisha kama wale binaadamu wenzetu walio katika kambi ile wanakaa katika mazingira kidogo ya kuridhisha, kwa sababu Mhe. Spika, hata ile Ofisi yao ni chini ya mizizi ya miembe ndipo walipo, hawana jengo hata la kujificha mvua pale.

Kwa hivyo, ni hatua gani za dharura ambazo Mhe. Waziri atazichukua ili kuhakikisha kama wale wenzetu walioko kule wanapata pahali pa kujihifadhi wakati huu ambapo jengo halijamalizika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Kama nilivyojibu suala mama kwamba Chuo cha Mafunzo baada ya kumaliza kujenga jengo la kuishi wanafunzi, ndipo hapo litachukua hatua ya kuweza kujenga jengo la utawala kwa wale askari wanaowatunza wanafunzi pale.

Lakini jengo litamalizika lini? Jengo tunatarajia limalizike katika kipindi cha Mwezi wa Julai, ifikapo Agosti mosi tunataka wanafunzi tuliowapeleka katika Gereza la Wete tuwarejeshe Kengeja.

**Nam. 45**

**Kukosekana kwa Pump Kwenye Josho la Mifugo Kisakasaka**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** **-** Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu kwa dakika moja tu kabla ya kuuliza Suala namba 45 kuchukua fursa hii kumshukuru Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuwafaraji wananchi waliopatwa na maafa na vile vile nitakuwa sijafanya haki kama sikumshukuru Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif na vile vile nitakuwa sijafanya haki kama sikumshukuru Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balosi Seif Ali Iddi na watendaji wake katika kuwafaraji na kuwapa pole akiwemo Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, rafiki yangu.

Baada ya maelezo hayo naomba Serikali itoe majibu ya suala Na. 45.

Kwa muda mrefu josho la mifugo la Kisakasaka limekuwa halifanyi kazi kutokana na kukosekana kwa "*pump*" na kusababisha mifugo kuchinjwa bila ya kusafishwa na dawa, jambo ambalo linaweza kusababisha maradhi ya mifugo na kuathiri wafugaji wetu Zanzibar.

(a) Serikali kwanini imeshindwa kuondoa tatizo hilo karibu nusu mwaka sasa na kusababisha mifugo kuendelea kuchinjwa bila ya kudhibitiwa maradhi ya mifugo.

(b) Ni lini Serikali itarudisha huduma hiyo badala ya josho hilo kuendelea kubaki kama pambo kinyume na azma ya kujengwa kwake.

(c) Mifugo inayoingia Kisakasaka inakaguliwa vipi kabla ya kuchinjwa ili kudhibiti maradhi ya kuambukiza.

**Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 45 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Josho la Karantini ya Kisakasaka hivi sasa linafanyakazi tokea mwezi wa Machi, 2015 baada ya kusafishwa na kujazwa maji mapya na dawa ya kupe (*phalanx)* na vidugu vyengine vinavyouliwa na dawa hiyo.

Mhe. Spika, Kwa maana hiyo ngombe wote na mbuzi wanaoingizwa nchini kupitia Kisakasaka waendelea kupata huduma ya kuogeshwa kwa lengo la kuuwa kupe na vidudu vyengine vya ngozi.

Mhe. Spika, kwa mwezi wa Marchi jumla ya ng'ombe 177, mwezi wa April, 2015 ng'ombe 65 waliogeshwa katika josho hili kutegemea na idadi ya wanyama wanaoingizwa nchini kwa mwezi husika.

Mhe. Spika, pampu kwa ajili ya kusafisha josho hili tayari imeshanunuliwa na inafanya kazi. Lakini vile vile kuna aina mbili ya malengo ambayo wanyama huingizwa nchini au hupitia Kisakasaka na namna yenyewe ni kama ifuatavyo.

Lengo la kwanza mifugo hii huingizwa nchini kwa sababu ya kuchinjwa. Mifugo hii inapingizwa, nataka nitoe taarifa tu kwa Baraza lako Tukufu, kuwa inapoingizwa mifugo hii huwekwa sehemu huoshwa na hufanyiwa aina zote za kutizamwa kama inafaa kwa kumlinda mlaji ama laa. Daktari anapothibitisha hili siku ya pili wanapelekwa kwenye chinjio na kuchinjwa na baadae kutizamwa nyama ile kama kweli inafaa au haifai. Kama inafaa ndio hutolewa pale, lakini si vyenginevyo kama anaweza kukoshwa au anaweza kuchinjwa bila ya kukoshwa.

Lakini lengo la pili ni kuingizwa nchini kwa sababu ya kufugwa, ili huhifadhiwa pale walipo wakisha kupewa dawa, lakini wakishakutoka kwenye Karantini wanakabidhiwa wenyewe na kwenda sehemu husika ambao watafugwa kule na kuleta manufaa kwa wafugaji.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana aliyojibu Mhe. Naibu Waziri vile vile akiwa Mwakilishi na kukidhi suali la msingi, naomba kumuuliza masuali mawili madogo tu ya nyongeza.

Hivi karibuni vyombo vya habari kama *ZBC* vilikariri kwa kuwa kuna tatizo kubwa la pampu katika chinjio hili na hivi sasa nikushukuru sana kwa kusema kwamba pampu hiyo tayari ipo na inafanya kazi.

1) Mmejipanga vipi juu ya kuweka pampu nyengine ya hakiba ili lisije likatokezea tena tatizo kama hili. Ukizingatia chinjio hili ni muhimu kwa wananchi wa Kisiwa hichi cha Unguja.

2) Pili, nikuombeni kama nyiye ndio wasimamizi wa machinjio, kwa nini hamkai na Baraza la Manispaa mkachukua lile chinjio la kuku kule Marikiti kutokana na hali yake ilivyokuwa, haliridhishi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, ni kweli kabisa nikubaliane nawe kuwa vyombo vyetu viliripoti hivyo, lakini kutokana tu na ukosefu wa mawasiliano uliokosa kuripotiwa Wizarani, ndio iliyosababisha kuonekana pampu ile wakati ule haifanyi kazi.

Na ni kweli pampu iliharibika, lakini kuna hatua hii ambayo tuliichukua kwa maramoja. Hatua yenyewe tulichukua gari la Manispaa likenda likanyonya yale maji ambayo yaliyokuwa yana taka, yakapeleka katika *stock tank* letu tukasafisha na tukatia dawa nyengine ya *peranets* na sasa hivi linafanya kazi. Lakini hili suala lako la kushirikiana na Manispaa ni vyema hata tumeliona mantiki yake tutalifanyia kazi.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa Mkoa wa Kaskazini Unguja ni miongoni mwa Mkoa ambao kuna Bandari, na Bandari hii inasafirisha wanyama wengi wakiwemo ng'ombe, mbuzi na hakuna hadhari yoyote ambayo inachukuliwa kuweza kupatiwa madawa wanyama hawa wakati wanaposhuka.

Je, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inawapatia huduma wanyama pale wanaposhushwa ili kuepusha maambukizi kwa wanyama wengine na pia usalama kwa wanadamu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, ni kweli kabisa kuna Bandari Kaskazini ambazo wanyama wengi hupitia kule, serikali tayari imechukua na imeona suala hilo na sasa sehemu ya Donge Muwanda, kuna Karantini ambayo tumeweka. Lakini hata katika Mkokotoni kuna madaktari wetu na tunayo sehemu tunaweka kwa dharura ile mpaka ile Karantini yetu ya Donge Muwanda itakapomalizika.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi leo kwa kuniona kuuliza suali hili la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri alisema kwa mwezi wa Marchi ng'ombe 177 ambao wameingizwa. Lakini vile vile kuingizwa kwa ng'ombe hao ni kwa ajili ya kuchinjwa na kwa ufugaji. Je, nimuulize Mhe. Waziri pamoja na ng'ombe hao kuingizwa 177 kuna ng'ombe wangapi ambao wamebainika kuwa hawafai kwa matumizi ya binaadamu. Ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, kipindi cha miaka mingi sasa hatujagundua ng'ombe yoyote ambaye hafai kwa kuliwa, wote mpaka sasa wapo sawa na tunaendelea vizuri na hatua ya nyama kukaguliwa inaendelea kila mara.

**Mhe. Spika:** Naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora.*(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Uwasilishaji wa Uchumi kwa Mwaka 2014 na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2015/2016

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kujadili na hatimae kuidhinisha hali ya uchumi kwa mwaka 2014 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2015/2016. Sambamba na Hotuba hii, nawasilisha vitabu 2; cha Kwanza cha taarifa ya hali ya uchumi kwa Mwaka 2014 na mwelekeo wa hali ya uchumi mwaka 2015. Kitabu cha pili kuhusu mapitio ya mpango wa maendeleo ya mwaka 2014/2015 na mwelekeo wa mpango wa maendeleo kwa mwaka 2015/2016. Taarifa zote hizi zimezingatia utekelezaji wa dira ya maendeleo ya 2020 ya Zanzibar, mkakati wa kukuza uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015 pamoja na Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

Mhe**.** Spika, naomba nitangulize hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, muumba wa vyote viliomo mbinguni na ardhini, ikiwa ni pamoja na sisi waja wake. Namshukuru kwa kutupa uhai, afya na uwezo na kukutana tena katika shughuli hii muhimu katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu nchi yetu na wananchi wake.Naomba Bwana Mola atuzidishie sote hekima na busara katika mijadala ya kikao hichi, atujaalie kheri, baraka na maelewano kati yetu. Atupe pia utulivu, upendo na mshikamano miongoni mwetu. Bila ya yeye, hatuna nguvu wala uwezo wa kufanya lolote.

Mhe. Spika, kwa unyenyekevu naomba kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tume ya

Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umakini wake katika uongozi wa nchi yetu. Hekima, busara na jitihada zake zimeendelea kuiweka nchi hii katika utulivu na amani kubwa, huku kukiwa na matumaini ya kufanya vizuri zaidi siku za usoni, kama Hotuba yangu hii itavyofafanua. Uongozi na maelekezo anayotupatia ndio chimbuko la hali hii njema ya Uchumi kwa mwaka 2014 na kuweza kuwa na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2015/2016 unaotia matumaini ambapo taarifa zake nitaziwasilisha mbele yenu.

Aidha, nachukua fursa hii kuwapongeza wasaidizi wakuu wa Mhe. Rais, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais kwa ushauri wao na kufanya kazi karibu zaidi na Mhe. Rais. Kutokana na umakini wa viongozi wetu hawa nchi yetu inakamilisha miaka mitano ya awamu ya saba kukiwa na utulivu mkubwa. Halikadhalika, kutokana na umakini wao kwa Mheshimiwa Rais, nchi imezidi kupiga hatua kimaendeleo kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mipango na programu za maendeleo. Naomba pia kuwashukuru wajumbe wote wa Tume ya Mipango kwa uadilifu wao na miongozo wanayotupatia katika utayarishaji, utekelezaji na usimamizi wa Mipango na Uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba sasa nikushukuru wewe Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Pandu Ameir Kificho, kwa kuendesha vyema vikao vya Baraza letu. Hilo lisingewezekana bila ya ushirikiano, hekima na busara za wasaidizi wako wote akiwemo Mhe. Ali Abdalla Ali, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Mgeni Hassan Juma–Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi na Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa–Mwenyekiti pia wa Baraza la Wawakilishi. Hekima, busara na uoni wenu vimesaidia sana katika kuishauri Serikali na kuifanya iwajibike vyema zaidi kwa wananchi wake. Hapana shaka kazi yenu kubwa ya kuliendesha Baraza kwa demokrasia na uwazi na mlifanya vizuri na kwa umakini mkubwa.

Aidha, kwa nafasi ya kipekee naishukuru Kamati ya Wenyeviti ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyo chini ya uongozi wa Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa maoni na ushauri waliotupatia. Nakiri kuwa wametusaidia kuifanya taarifa hii ninayoiwasilisha hapa leo kuwa bora zaidi. Tunaahidi kuwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itaendelea kushirikiana na Kamati hii kwa mustakabali mzuri wa kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, naomba kwa mara nyengine kutumia fursa hii kutoa mkono wa pole kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote kwa kuondokewa hivi karibuni na mwenzetu aliyetangulia mbele ya haki, Marehemu Salmin Awadh Salmin aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni na Mnadhimu wa Chama Cha Mapinduzi. Natoa pole kwa familia ya marehemu,

ndugu na wananchi wa Jimbo la Magomeni. Aidha, tunamuomba Mwenyezi Mungu awarehemu Waheshimiwa Wawakilishi wengine waliotangulia mbele ya haki kabla yake. Sote ni wa Mwenyenzi Mungu, na sote tutarejea kwake.Tunaungana na familia zao kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu wepesi wa kurudi kwao na malazi mema Peponi. *Amin*.

Mhe. Spika, kutokana na uongozi wa busara wa viongozi wetu wakuu, usimamizi mzuri wa Baraza lako Tukufu, utekelezaji mzuri wa watendaji wetu wa Serikali na wananchi wote wa Zanzibar, uchumi wetu kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2010–2014 ulikuwa kwa kiwango cha kuridhisha cha wastani wa asilimia 6.5. Ukuaji huu ulitokana na kuimarika kwa sekta ndogo ya ujenzi, sekta ndogo ya fedha na bima, sekta ndogo ya usafiri, sekta ndogo ya habari na mawasiliano na kuimarika kwa sekta ndogo ya utawala wa umma. Aidha, idadi ya watu inakadiriwa kuwa 1,375,000 mwaka 2014. Hivyo, Pato la Wastani la kila mtu kwa kipindi cha miaka mitano limefikia wastani wa TZS 1.3 milioni (*USD* 774). Hali hii inaashiria kiwango cha ukuaji wa shughuli za uchumi kwenda sambamba na ukuaji wa pato la mtu binafsi.

Mhe. Spika, mwaka 2015 ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu ya Zanzibar na vile vile kwa maendeleo ya kidunia. Kwa upande wa Zanzibar ni mwaka ambao tunatarajia kuanza mapitio ya MKUZA II ambayo yaliakhirishwa kutokana na kusubiri kukamilika utafiti wa mapato na matumizi ya Kaya yaliyoanza mwaka 2014. Viashiria vinavyotokana na utafiti huu ni muhimu na ndiyo vinavyotumika kupima mafanikio ya utekelezaji wa MKUZA II. Serikali pia imo katika kufanya utafiti wa kujua nafasi iliopo kiuchumi Zanzibar *(Zanzibar Economic Position Paper),* utafiti huu una umuhimu mkubwa katika kuendeleza sekta za kiuchumi na kijamii.

Aidha, kidunia, mataifa yanasubiri kwa hamu malengo endelevu ya maendeleo ambayo yatachukua nafasi ya malengo ya maendeleo ya milenia yanayomaliza muda wake mwaka 2015. Malengo hayo mapya yatahitaji kuingizwa katika mipango ya nchi, ikiwemo awamu mpya ya MKUZA inayotarajiwa kukamilika mwaka 2016.

Mhe. Spika, mwaka 2015 ni mwaka ambao Zanzibar inatarajia kufanya uchaguzi mkuu ifikapo Oktoba 2015. Kama tunavyofahamu kuwa uchaguzi ni moja ya nguzo muhimu katika maendeleo ya demokrasia katika nchi ambayo inajali sheria na utawala bora. Hivyo wito wangu kwa wananchi ni kuingia katika uchaguzi kwa hali ya amani na utulivu, bila ya kuathiri uchumi na maendeleo ya nchi kwa jumla. Hivyo, nachukua fursa hii kuwatakia wananchi wote utekelezaji mzuri wa jukumu hili muhimu kwa utulivu ili tukamilishe zoezi la uchaguzi kwa salama na hatimaye tukutane katika Baraza hili muhimu kuendelea kuisimamia vyema serikali yetu.

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/15 umekumbwa na changamoto kadhaa ambazo zimeathiri utekelezaji wake. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:

(a) Kusita kwa washirika wa maendeleo kutoa fedha za misaada ya kibajeti (*GBS*). Hali hii imesababishwa na mgogoro wa akaunti ya "*ESCROW*" na kupelekea kutotekelezwa kwa baadhi ya miradi ya maendeleo kwa mwaka huu;

(b) Kudhoofika kwa thamani ya sarafu ya Tanzania kulikopelekea kuongezeka kwa thamani ya dhima zinazolipwa kwa fedha za kigeni.

Mhe. Spika, hotuba yangu ya leo imegawika katika sehemu kuu tano.

1. Mapitio ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2014;

2. Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa kwa mwaka 2014/2015;

3. Mwelekeo wa Hali ya Uchumi mwaka 2014;

4. Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2015/2016; na

5. Hitimisho.

## MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2014

### Hali ya Uchumi Duniani

### Ukuaji wa Uchumi

Mhe. Spika, uchumi wa dunia kwa mwaka 2014 haukuwa na mabadiliko na umeendelea kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 3.4, sawa na mwaka 2013. Uchumi wa nchi zilizoendelea umekua kwa wastani wa asilimia 1.8 kwa mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 1.4 kwa mwaka 2013. Nchi zinazoibukia na zinazoendelea uchumi wake umekua na kufikia wastani wa asilimia 4.6 kwa mwaka 2014 kutoka asilimia 5.0 mwaka 2013. Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ukuaji wake umefikia asilimia 5.0 mwaka 2014 kutoka asilimia 5.2 mwaka 2013. Ukuaji huu unatokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi za Ulaya, mabadiliko ya hali ya hewa, kuendelea kushuka kwa bei za mafuta duniani na kupungua kwa uzalishaji viwandani. Aidha, kwa baadhi ya nchi za

Kusini mwa Jangwa la Sahara umechangiwa pia kwa kuibuka kwa maradhi ya Ebola.

**Mwenendo wa Mfumko wa Bei Duniani**

Mhe. Spika, Kasi ya mfumko wa bei duniani kwa mwaka 2014 imefika asilimia 3.5 kutoka asilimia 3.9 mwaka 2013. Kwa nchi zilizoendelea, kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2014 imefikia asilimia 1.3 kutoka asilimia 1.2 mwaka 2013. Aidha, kwa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi mfumko wa bei umeshuka kufikia asilimia 5.1 mwaka 2014 kutoka asilimia 5.9 mwaka 2013. Kushuka kwa bei za vyakula, kuendelea kushuka kwa bei za mafuta duniani na kuwepo kwa sera madhubuti za kifedha ndio sababu zilizopelekea kupungua kwa kasi ya mfumko wa bei kwa nchi hizi.

**Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar**

Mhe. Spika, serikali imefanya Mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa kwa kubadilisha mwaka wa kizio kutoka 2001 na kwenda 2007. Kazi hii ilihusisha mabadiliko ya njia za kufanyia hesabu na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa takwimu kwa kuzingatia maelekezo ya Umoja wa Mataifa.

Mhe. Spika, aidha, mapitio yaliingiza takwimu mpya zilizotokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya ya mwaka 2004/2005 na wa mwaka 2009/2010, Sensa ya Kilimo ya mwaka 2003/2004 na ya mwaka 2007/2008, Sensa ya Uzalishaji Viwandani ya mwaka 2008, Utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanyakazi wa mwaka 2006, Utafiti mdogo kwa sekta ya ujenzi, biashara na usafirishaji wa mwaka 2010 na utafiti wa sekta ya uvuvi wa mwaka 2012.

Mhe. Spika, mabadiliko haya yaliofanyika yanatarajiwa kuimarisha takwimu za viashiria vya uchumi mkuu na kuonesha maendeleo ya kiuchumi nchini. Viashiria vipya vilivyoongezeka ni pamoja na taaluma, ufundi na sayansi; utawala na utoaji huduma; sanaa na burudani; na huduma za majumbani.

**Ukuaji wa Pato la Taifa**

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014, Pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 7.2 mwaka 2013. Ukuaji huu wa Pato la Taifa umechangiwa zaidi na mambo yafuatayo:

i) Kuimarika kwa sekta ya huduma ambayo imekua kutoka asilimia 4.6 mwaka 2013 hadi asilimia 9.8 mwaka 2014. Shughuli ambazo zilikuwa kwa kasi ni fedha na bima asilimia 10.6, habari na mawasiliano asilimia 24.5, biashara na

ukarabati asilimia 13, makaazi asilimia 8.7, utawala asilimia 10.8 na afya na huduma ya jamii asilimia 7.4;

ii) Kuimarika kwa sekta ya viwanda ambayo imekua kutoka asilimia 3.5 mwaka 2013 hadi asilimia 6.0 mwaka 2014. Shughuli ambazo zilikua kwa kasi ni uchimbaji wa mawe asilimia 4.9, uzalishaji viwandani asilimia 9.6, umeme na gesi asilimia 4.7 na ujenzi asilimia 3;

iii) Kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini kutoka watalii 181,301 mwaka 2013 hadi kufikia watalii 311,891 mwaka 2014; na

iv) Kuwepo kwa hali ya amani na utulivu.

Mhe. Spika, kasi ya ukuaji katika sekta ya kilimo imeshuka kidogo kwa asilimia 0.4 mwaka 2014 kutoka asilimia 13.2 mwaka 2013. Hali hii imesabishwa na kushuka kwa sekta ndogo ya mazao iliyofikia asilimia 7.2 mwaka 2014 kutoka asilimia 22.9 mwaka 2013 na kupungua kwa ekari zilizozalishwa mazao kwa asilimia 7 kutoka ekari 94,701 mwaka 2013 hadi ekari 87,944 mwaka 2014.

Mhe. Spika, Upungufu huu umetokana na kupungua ekari zilizopandwa mpunga kutoka ekari 34,721 zilizozalisha tani 33,655 mwaka 2013 hadi ekari 30,535 na kuzalisha tani 29,564 mwaka 2014. Vile vile, kupungua ekari zilizopandwa muhogo kutoka ekari 27,995 na kuzalisha tani 164,332 mwaka 2013 hadi ekari 27,036 na kuzalisha tani 158,704 mwaka 2014 na migomba kutoka ekari 8,545 zilizozalisha tani 68,358 za ndizi mwaka 2013 hadi ekari 6,679 zilizozalisha tani 57,437 za ndizi mwaka 2014.

Hata hivyo, sekta ndogo ya mifugo ilikuwa kwa asilimia 7.5 mwaka 2014 kutoka asilimia 5.1 mwaka 2013, uvuvi ulikuwa kwa asilimia 8.9 mwaka 2014 kutoka asilimia 3.6 mwaka 2013 ambapo upatikanaji wa samaki umeongezeka kutoka tani 30,712 zenye thamani ya TZS 111.87 bilioni hadi tani 32,974 yenye thamani ya TZS 127.21 bilioni na uzalishaji wa mazao ya misitu ulikuwa kwa asilimia 3.8 mwaka 2014 kutoka asilimia 3.5 mwaka 2013.

Sababu zilizopelekea kupungua kwa uzalishaji wa mazao ni kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, kupungua kwa ekari za eneo zinazolimwa muhogo, mpunga na migomba; kubadilisha mwelekeo kwa baadhi ya wakulima kuacha kilimo cha mazao ya chakula kwenda mazao ya matunda na mboga mboga na kujitokeza kwa maradhi ya migomba na muhogo pamoja na wadudu waharibifu katika muhogo na mipapai.

**Pato la Mwananchi**

Mhe. Spika, Pato la Taifa kwa Zanzibar lilifikia thamani ya TZS 2,133.5 bilioni mwaka 2014 kutoka thamani ya TZS 1,849.9 bilioni kwa mwaka 2013. Kuongezeka kwa Pato la Taifa kwa zaidi ya ongezeko la watu kumepelekea kupanda kwa kiwango cha wastani wa Pato la kila mtu. Wastani wa Pato kwa kila mtu limeongezeka kutoka TZS 1,384,000 (*USD* 866) mwaka 2013 hadi TZS 1,552,000 (USD 939) mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 12.1.

**Mchango wa Sekta mbali mbali katika Pato la Taifa**

**Sekta ya Kilimo**

Mhe. Spika, mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa kwa mwaka 2014 umefikia asilimia 27.9 kutoka asilimia 30.4 mwaka 2013. Hali hii imesababishwa na kupungua kwa mchango wa sekta ndogo ya mazao kutoka asilimia 18.0 mwaka 2013 hadi asilimia 15.9 mwaka 2014. Aidha, mchango wa sekta ya mifugo umepungua kutoka asilimia 3.1 mwaka 2013 kufikia asilimia 2.8 mwaka 2014 na mchango wa sekta ya uvuvi umepungua kutoka asilimia 6.5 mwaka 2013 hadi asilimia 6.4 mwaka 2014 na mchango wa sekta ya misitu ulibaki kuwa asilimia 2.8 mwaka 2014 kama ilivyokua mwaka 2013.

**Sekta ya Viwanda**

Mhe. Spika, mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa umefikia asilimia 16.8 mwaka 2014 kutoka asilimia 18.0 mwaka 2013. Kupungua kwa mchango wa sekta ya viwanda kumetokana na kupungua kwa mchango wa sekta ndogo ya uzalishaji viwandani kutoka asilimia 7.0 mwaka 2013 hadi kufikia asilimia 6.4 mwaka 2014, sekta ndogo ya ujenzi nayo pia imepungua kutoka asilimia 8.5 mwaka 2013 na kufikia asilimia 7.9 mwaka 2014 na kupungua kwa mchango wa sekta ndogo ya umeme na gesi kutoka asilimia 0.4 mwaka 2013 hadi asilimia 0.3 mwaka 2014. Aidha, mchango wa sekta ndogo ya uchimbaji mawe kwa mwaka 2014 umeendelea kubaki asilimia 1.5.

**Sekta ya Huduma**

Mhe. Spika, mchango wa sekta ya huduma katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 41.5 mwaka 2013 hadi kufikia asilimia 44.7 mwaka 2014. Kuongezeka huko kumetokana na kuongezeka kwa mchango wa sekta ndogo ya habari na mawasiliano kutoka asilimia 1.3 mwaka 2013 hadi asilimia 5.4 mwaka 2014, kuongezeka kwa mchango wa sekta ndogo ya taasisi za fedha na bima kutoka asilimia 3.4 mwaka 2013 kufikia asilimia 4.1 mwaka 2014, pia kuongezeka

kwa mchango wa sekta ndogo ya uwekezaji katika majengo kutoka asilimia 6.1 mwaka 2013 hadi asilimia 6.9 mwaka 2014 na sekta ndogo ya taaluma, ufundi na sayansi kuongezeka kutoka asilimia 0.3 mwaka 2013 hadi asilimia 0.4 mwaka 2014.

**Mfumko wa Bei**

Mhe. Spika, kasi ya mfumko wa bei kwa bidhaa na huduma imepanda kutoka asilimia 5.0 mwaka 2013 kufikia asilimia 5.6 mwaka 2014. Kasi hii ya kupanda kwa mfumko wa bei nchini ilichangiwa na kupanda kwa mfumko wa bei za chakula (hasa samaki na ndizi) kutoka asilimia 1.8 mwaka 2013 hadi asilimia 4.4 mwaka 2014. Hata hivyo, kwa bidhaa zisizo za chakula kasi ya mfumko wa bei imeshuka kutoka asilimia 8.5 mwaka 2013 hadi asilimia 6.8 mwaka 2014 (hasa bidhaa za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa).

**SEKTA YA NJE**

**Biashara na Nchi za Nje**

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014, mwenendo wa biashara na nchi za nje umeimarika kutokana na kuongezeka kwa thamani ya usafirishaji wa bidhaa na huduma. Hata hivyo, nakisi ya biashara imefikia asilimia 21.3 kutoka nakisi ya thamani ya TZS 120.3 bilioni mwaka 2013 hadi nakisi ya thamani ya TZS 146.0 bilioni kwa mwaka 2014.

Mhe. Spika, thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi pia iliongezeka kutoka TZS 87.8 bilioni mwaka 2013 kufikia thamani ya TZS 133.6 bilioni mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 53. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa mazao ya biashara (karafuu, mwani na makonyo) kutoka thamani ya TZS 75.4 bilioni mwaka 2013 hadi thamani ya TZS 103.9 bilioni mwaka 2014.

Mhe. Spika, kwa upande wa uagiziaji wa bidhaa kutoka nje, thamani imeongezeka kwa asilimia 34.4 kutoka TZS 208.1 bilioni mwaka 2013 hadi kufikia thamani ya TZS 279.6 bilioni mwaka 2014. Kwa mwaka 2014 uagiziaji mkubwa ulikuwa katika vyombo vya usafiri na mashine.

**Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara**

Mhe. Spika, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umefikia thamani ya TZS 64.3 bilioni mwaka 2014 kutoka thamani ya TZS 61.8 bilioni mwaka 2013 na uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara

umefikia thamani ya TZS 366.4 bilioni mwaka 2014 kutoka thamani ya TZS 501.2 bilioni mwaka 2013.

**Mwenendo wa uingiaji wa Watalii**

Mhe. Spika, katika mwaka 2014 sekta ya utalii imezidi kuimarika kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka 181,301 mwaka 2013 kufikia watalii 311,891 mwaka 2014. Mwenendo huu mzuri wa watalii umetokana na kuimarika kwa ukusanyaji wa takwimu za watalii na kuimarika kwa huduma mbali mbali zilizopelekea kuongezeka kwa idadi ya watalii ikiwemo kuongezeka kwa hoteli za daraja la juu (nyota 5) katika Mkoa wa Mjini Magharibi na Kaskazini Unguja kutoka hoteli 3 mwaka 2013 kufikia hoteli 7 mwaka 2014. Vile vile, kupungua kwa msukosuko wa uchumi na fedha uliozikumba nchi za Ulaya kuanzia mwaka 2012, hali iliyopelekea kuongezeka kwa watalii kutoka Bara la Ulaya kwa asilimia 61.4 kufikia watalii 191,641. Aidha, watalii kutoka Bara la Asia walifikia 25,279 sawa na asilimia 8.1, watalii kutoka Bara la Afrika walifikia 35,308 sawa na asilimia 11.3, watalii kutoka Marekani walifikia 29,451 sawa na asilimia 9.4.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, ipo haja ya kuitangaza zaidi Zanzibar katika nchi zenye idadi ndogo ya uingiaji wa wageni ili kuepukana na kutegemea watalii kutoka sehemu moja ambapo inaweza kuleta athari za uchumi nchi hizo zinapopata matatizo.

**UKUZAJI RASILIMALI**

Mhe. Spika, kwa ujumla thamani ya ukuzaji rasilimali imepungua kwa asilimia 7.8 kutoka TZS 515.8 bilioni mwaka 2013 hadi TZS 475.4 bilioni mwaka 2014. Hii imetokana na kupungua kwa uwekezaji katika eneo la vifaa vya ujenzi kutoka thamani ya TZS 353.2 bilioni mwaka 2013 hadi TZS 288.6 bilioni mwaka 2014. Hata hivyo, thamani ya uwekezaji wa vifaa vya usafirishaji imeongezeka kutoka TZS 68.8 bilioni mwaka 2013 hadi TZS 79.1 bilioni kwa mwaka 2014 na vifaa vyenginevyo kutoka TZS 86.7 bilioni mwaka 2013 hadi TZS 99.7 bilioni mwaka 2014.

**UWEKEZAJI BINAFSI**

Mhe. Spika, sekta binafsi ni sekta mojawapo inayounga mkono juhudi za Serikali katika kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa lengo la kuharakisha maendeleo ya Taifa. Sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kutoa ajira, kuongeza uzalishaji, kupunguza utegemezi kutoka mataifa ya nje na kuingiza teknolojia mpya.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka 2014, Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*) ilisajili miradi 26 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 526.71 ambapo mradi mmoja uko katika hatua za ujenzi. Kwa mwaka 2013 miradi iliayosajiliwa ilikuwa ni 35 yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 1,061.9 ambapo miradi mitatu ilikuwa katika hatua ya ujenzi. Sekta ndogo ya hoteli na mikahawa imeongoza kuwa na miradi mingi zaidi ikilinganishwa na miradi mengine. Kwa mwaka 2014 imefikia miradi 10 kutoka miradi 16 mwaka 2013. Kushuka kwa uwekezaji katika sekta ya hoteli kumetokana na wawekezaji wenyewe kuangalia sekta nyengine za uwekezaji. Sekta hizo ni pamoja na ukodishaji wa nyumba za biashara na shughuli za biashara.

Mhe. Spika, Sekta ya Ukodishaji wa majumba na shughuli za biashara ziliongezeka kutoka miradi 7 yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 128.1 mwaka 2013 hadi kufikia miradi 9 yenye thamani ya dola za kimarekani 166.8 mwaka 2014. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 28.6 ya idadi ya miradi, sawa na ongezeko la asilimia 30.2 ya thamani ya miradi. Miradi hiyo ilitoa fursa za ajira 972 mwaka 2014 ambazo ni upungufu wa asilimia 28.8 ikilinganishwa na fursa za ajira 1,365 kwa mwaka 2013. Hata hivyo, fursa za ajira za biashara za mauzo ya jumla na reja reja ziliongezeka kufikia 230 mwaka 2014 na miradi ya huduma za afya ya jamii zilifikia 82 kwa mwaka 2014.

## SEKTA YA FEDHA

### Huduma za Benki

Mhe. Spika, sekta ya fedha imezidi kuimarika katika mwaka 2014/15. Amana za benki ziliongezeka kwa asilimia 12.4 kutoka TZS 477.7 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kilichoishia mwishoni mwa mwezi Machi 2014 kufikia TZS 536.8 bilioni mwezi Machi 2015. Hali hii inaashiria kuwa watumiaji wa huduma za kibenki wanaongezeka kutokana na uhamasishwaji unaotokana na ushindani wa benki ukiambatana na kuimarika kwa huduma za Benki ya Kiislamu na huduma za kibenki kupitia simu za mikononi.

Mhe. Spika, Mikopo kwa sekta binafsi kwa upande mwengine, imeongezeka kwa asilimia 1.0 kutoka TZS 203.8 bilioni mwezi wa Machi 2014 na kufikia TZS 205.8 bilioni katika kipindi kilichoishia mwezi Machi 2015. Uwiano wa mikopo na amana ulifikia asilimia 38.3 kutoka asilimia 42.7 kutokana na tahadhari ambazo benki zinachukua wakati wa kukopesha, kwani urejeshwaji wa mikopo iliyo mingi sio wa kuridhisha pamoja na usimamishaji wa kutoa mikopo kwa muda kwa benki moja ambayo inafanyiwa marekebisho.

Mhe. Spika, uchambuzi wa mikopo kwa walionufaika nao unaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2015, jumla ya mikopo iliyotolewa ilifikia TZS 205.8 bilioni, ambapo mikopo katika miradi binafsi ilifikia asilimia 39.3, biashara asilimia 16.7, utalii asilimia 13.4, sekta zilizobakia zilipokea mikopo chini ya asilimia 2 kila moja, zikiwemo kilimo na viwanda ambazo hutoa mchango mkubwa katika uchumi. Sababu zinazopelekea mikopo kupungua katika sekta ya kilimo ni pamoja na ukosefu wa dhamana ambazo benki inazikubali, hii ni kutokana na sekta ya kilimo kutegemea zaidi hali ya hewa na hivyo mabenki kuweka masharti makubwa zaidi ya mikopo katika sekta hii.

Mhe. Spika, wastani wa viwango vya riba kwa kuweka amana katika benki vilipanda kutoka asilimia 4.2 mwezi Machi, 2014 hadi kufikia asilimia 4.4 katika kipindi kilichoishia mwezi Machi, 2015. Wakati wastani wa riba zinazotokana na mikopo ulipungua kutoka asilimia 16.5 hadi kufikia asilimia 16.3 katika kipindi hiki. Hali hii ilipelekea tofauti baina ya viwango vya riba za kuweka na kukopa kupungua kutoka asilimia 12.3 Machi, 2014 mpaka kufikia asilimia 12.0 katika kipindi kilichoishia mwezi Machi, 2015.

**THAMANI YA FEDHA YA TANZANIA**

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014 thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani ilishuka kwa wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na kushuka kwa asilimia 1.7 mwaka 2013. Hali hii imetokana na kuwepo kwa mahitaji makubwa ya Dola ya Kimarekani kutokana na kusimamishwa kwa misaada ya kibajeti (*GBS*) na kupungua kwa uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya biashara ya Tanzania. Vile vile, kuimarika kwa sarafu ya dola ya Kimarekani ukilinganisha sarafu nyengine maarufu ulimwenguni (*Euro, Pound Sterling na Yen*).

**MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI**

Mhe. Spika, mapato ya ndani kwa mwaka 2013/14 yalikuwa ni TZS 330.7 bilioni sawa na asilimia 17.9 ya Pato la Taifa. Aidha, matumizi yalikuwa TZS 371.1 bilioni sawa na asilimia 20.1 ya Pato la Taifa. Hivyo, nakisi ya bajeti, ikijumuisha misaada ilikuwa asilimia 7.7 ya Pato la Taifa katika mwaka 2013/2014. Mwaka 2014/2015 Serikali ilikadiria kukusanya mapato ya ndani jumla ya TZS 386.8 bilioni sawa na asilimia 18.1 ya Pato la Taifa. Matumizi yanakadiriwa kuwa TZS 707.8 milioni sawa na asilimia 33.2 ya Pato la Taifa.

**MAENDELEO YA KIUCHUMI**

Mhe. Spika, kwa upande wa maendeleo ya kiuchumi, kuendelea kukua kwa uchumi nchini kumeenda sambamba na maendeleo ya kiuchumi na kuimarika kwa

ustawi wa wananchi. Juhudi mbali mbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini zimesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha hali na ustawi wa wananchi wa Zanzibar. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na hayo yafuatayo:

i) Kuongezeka kwa idadi ya wananchi waliounganishwa na huduma ya umeme katika Gridi ya Taifa kutoka watu 8,126 mwaka 2013 hadi kufikia watu 10,410 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 28;

ii) Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi walioorodheshwa katika shule za msingi za Serikali na binafsi kutoka 247,352 mwaka 2013 hadi kufikia 253,152 mwaka 2014. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 2.3;

iii) Wastani wa uwiano wa walimu kwa wanafunzi kwa darasa la kwanza mpaka kidato cha nne kwa skuli za Serikali na binafsi umeendelea kuwa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 26, sawa na mwaka 2013;

iv) Kuimarika kwa utoaji wa huduma katika sekta ya afya kwa kuongezeka kwa Madaktari ambao wamefikia Madaktari 142. Kwa idadi hii ya Madaktari na idadi ya watu wa Zanzibar, kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, Daktari mmoja anatoa huduma kwa watu 9,708 mpaka mwishoni 2014;

v) Idadi ya skuli za msingi na sekondari zimeongezeka kutoka 392 mwaka 2013 hadi 407 mwaka 2014 kwa skuli za Serikali na skuli 94 mwaka 2013 hadi skuli 99 mwaka 2014 kwa skuli za Binafsi; na

vi) Kuongezeka kwa wanafunzi waliopata mkopo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kutoka wanafunzi 881 iliyogharimu TZS 5.22 bilioni mwaka 2012/13 hadi wanafunzi 1,467 iliyogharimu TZS 6.42 bilioni mwaka 2013/14.

**MASUALA YA MTAMBUKA**

**i) Idadi ya Watu**

Mhe. Spika, idadi ya watu Zanzibar na kasi ya kuongezeka kwake inaendelea kuwa miongoni mwa maeneo yenye kupewa mazingatio katika mipango bora na

endelevu nchini. Taarifa zinaonesha kwamba kumekuwa na kasi ndogo ya ukuaji wa idadi ya watu. Kasi hiyo imefanya idadi ya watu kuongezeka kutoka watu 981,754 waliokuwa wakiongezeka kwa kasi ya asilimia 3.0 mwaka 2002 hadi 1,303,569 wanaongezeka kwa kasi ya asilimia 2.8 mwaka 2013. Ukuaji huu umepelekea mgawanyo wa watu kwa makundi mbali mbali kuwa sio rafiki katika juhudi za Serikali kupunguza umasikini na kuleta maendeleo husasan kutokanana kuongezeka kwa kiwango cha utegemezi.

Mhe. Spika, mgawanyo wa watu Zanzibar unaonyesha kwamba idadi kubwa ya watu ni wanawake waliofikia 672,892 sawa na asilimia 51.6 ikilinganishwa na wanaume 630,677 sawa na asilimia 48.4; idadi kubwa ya watu wa Zanzibar sawa na asilimia 68.8 wapo Kisiwani Unguja ikilinganishwa na Pemba yenye asilimia 31.2 ya Wazanzibari wote. Watu wengi zaidi kiasi cha asilimia 46 wapo katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Mgawanyo wa watu kiumri unaonyesha kwamba kiasi cha asilimia 65.6 ya Wazanzibari ni wale ambao kwa njia moja au nyengine wanahitaji usaidizi wa kimaisha kutoka kwa familia zao ikihusisha watoto chini ya miaka 15 (asilimia 42.5), vijana wenye umri wa miaka 15 - 24 (asilimia 20.3) na wazee wa miaka 65 na zaidi (asilimia 2.8).

Mhe. Spika, ukuaji wa kasi ndogo ya idadi ya watu wa asilimia 2.8 umetokana na juhudi za Serikali kuzingatia uingizaji wa viashiria vya idadi ya watu katika mipango ya sekta mbali mbali hususan afya iliyopelekea kupungua kwa kiwango cha uzazi na vifo vya kina mama na watoto. Taarifa zinaonyesha kwamba kiwango cha uzazi kwa kina mama wenye umri wa kuzaa kimepungua kutoka watoto 6.4 mwaka 1991 hadi watoto 5.1 mwaka 2012; vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka 120 mwaka 1988 hadi kufikia 46 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 2012; vifo vya watoto chini ya miaka mitano navyo vimeshuka kutoka 202 mwaka 1988 hadi 66 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 2012. Aidha, vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi navyo vimeshuka kutoka 377 mwaka 1988 hadi 307 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2012.

Mhe. Spika, mafanikio hayo yametokana na juhudi za Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo na asasi za kiraia kuelimisha jamii na kuimarisha huduma mbali mbali za afya ya uzazi kwa kinamama na watoto, hali ambayo imepelekea pia kupanda kwa umri wa kuishi wa Mzanzibari kufikia zaidi ya miaka 60. Hata hivyo, kasi iliyopo ya idadi ya watu imekuwa ni changamoto katika maeneo ya ajira kwa vijana, upatikanaji wa huduma mbali mbali za kijamii, matumizi yasio mazuri ya rasilimiali ardhi, misitu na kadhalika.

Serikali inaendeleza mikakati mbali mbali ili kukabiliana na hali hii. Mipango na mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha zaidi huduma za afya ya uzazi kwa kinamama na watoto katika hospitali na vituo vya afya, kuhuisha miji Zanzibar,

kuendelea na utekelezaji wa programu za ajira kwa vijana, kuimarisha na kuongeza vyuo vya amali nchini, kuendelea na mchakato wa uvuvi wa bahari kuu. Mikakati hiyo inajumuisha pia kuanzisha pensheni ya wote kwa jamii (*Universal Pension*) kwa wazee wa miaka 70 na zaidi, kuondoa michango ya elimu ya msingi na kuendelea kutoa mikopo ya elimu ya juu na kadhalika.

**ii) Ukimwi**

Mhe. Spika, Serikali imeendelea vyema na jitihada za kupambana na Ukimwi. Juhudi mbali mbali zimechuliwa katika kipindi cha 2010/2011 hadi 2014/2015 ikiwemo kutayarisha Mwongozo wa Pili wa Mapambano Dhidi ya Ukimwi. Sera imefanyiwa mapitio ili iweze kuoana na hali halisi ya maambukizi ya *VVU* na Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Ukimwi imetungwa mwaka 2013 ambayo inalinda haki ya watu wote kupata huduma na kutonyanyapaliwa kwa aina yoyote ile.

Mhe. Spika, tafiti mbali mbali zimefanyika ikiwemo afya ya uzazi na ukimwi pamoja na ukimwi kwa wavuvi. Uwezo wa jamii katika kupambana na ukimwi na ukatili kwa wanawake na watoto umeimarishwa kwa kujenga uwezo kwa kamati za Shehia ya kutoa elimu ya afya ya uzazi. Pia, Serikali imeendelea kutoa huduma rafiki za ukimwi kwa makundi maalum kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia mbali mbali. Aidha, mafunzo na semina zimetolewa kwa watoa huduma na viongozi wa kisiasa, taasisi za dini, *NGO's*, watu wanaoishi na *VVU* na kwa Wizara za Serikali.

**iii) Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi**

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2010/2011 hadi 2014/2015, Serikali katika kusimamia mazingira imezindua Sera Mpya ya Mazingira ya mwaka 2013 ambayo inatoa mwongozo kwa shughuli za uhifadhi wa mazingira na kuzingatia athari za mabadiliko ya tabia nchi, imetarayarisha sheria mpya ya mazingira ya mwaka 2015 inayotoa mfumo bora wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi wa mazingira. Aidha, Serikali imeendelea kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa kurusha vipindi vya radio, *TV* na kutumia filamu pamoja na kufanya mikutano kwa wananchi. Serikali pia imefanya mapitio ya miradi ya vitega uchumi kwa kufanya tathmini 71 za athari za kimazingira na kutolewa vyeti na miradi 221 imefanyiwa ufuatiliaji na kutolewa ushauri upasavyo.

Mhe. Spika, kuhusu kusimamia mabadiliko ya tabia nchi kutokana na ukubwa wa tatizo hili duniani, Zanzibar imeungana na nchi za dunia katika kukabiliana na kuhimili athari zake kwa kufanya utafiti wa kuangalia athari za mabadiliko ya tabia nchi kwa uchumi wa Zanzibar. Utafiti huo umebaini kuwa karibu sekta zote kuu za uchumi kwa njia moja ama nyengine zinaathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Tayari Serikali imeandaa mkakati wa Zanzibar wa mabadiliko ya tabia nchi, ambao unatoa dira ya hatua za Serikali na wadau wengine zinazotakiwa kuchukuliwa za kuihami na kuhimili na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

### iv) Maendeleo ya Jinsia na Kumwezesha Mwanamke

Mhe. Spika, tokea mwaka 2010 hadi sasa maendeleo makubwa yamepatikana kwa upande wa kukuza usawa wa kijinsia na kumwezesha mwanamke. Kwa upande wa kukuza usawa wa kijinsia, Serikali imeweza kukuza uwezo wa watendaji katika kuzingatia usawa wa kijinsia wakati wa kuandaa sera, mipango na bajeti. Vile vile, mwongozo wa kutayarisha bajeti kwa kuzingatia jinsia, kuunda kikundi kazi cha kuzingatia na kutekeleza sera, mipango na programu za kitaifa na kisekta kwa kuzingatia masuala na uwiano wa kijinsia.

Mhe. Spika, aidha, Serikali imepiga hatua nzuri katika kumwezesha mwanamke katika nyanja mbali mbali za uongozi na maamuzi. Katika jitihada za kumkomboa mwanamke kiuchumi, mfuko maalum wa kutoa mikopo nafuu kwa mwanamke umeanzishwa. Aidha, Mfuko wa Uwezeshaji unatoa mikopo midogo midogo kwa wanawake. Hadi mwezi Julai, 2014 kati ya mikopo 1,246 iliyotolewa, mikopo 679 ilimnufaisha mwanamke moja kwa moja. Aidha, hadi Disemba 2014, jumla ya vikundi 1,560 vya wanawake vimetambuliwa Unguja (981) na Pemba (670). Vile vile, Serikali imezindua kampeni ya miaka miwili ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kuandaa mpango wa miaka mitano wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

### v) Hali ya Ajira

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekua ikiendelea kuchukua juhudi mbali mbali kuhakikisha upatikanaji wa nafasi za ajira katika sekta tofauti unaimarika. Katika kuendeleza juhudi hizo ndani ya kipindi cha miaka minne iliyopita kutoka mwaka 2011/12 hadi mwaka 2014/15 jumla ya nafasi za ajira 25,019 zilizotolewa na kujazwa katika sekta mbali mbali serikalini (6,470 sawa na asilimia 25.9) na sekta binafsi (18,549 sawa na asilimia 74.1). Katika kipindi hicho cha miaka minne nafasi za ajira zilizozalishwa na kujazwa Serikali Kuu zimefikia 4,850. Idadi kubwa ya nafasi za umma zimepatikana katika mwaka 2014/15 zilizofikia 1,905 sawa na asilimia 39.3 na idadi ndogo ni katika mwaka 2011/12 ambapo jumla ya nafasi 330 za ajira zilijazwa sawa na asilimia 6.8.

Uchambuzi wa nafasi hizo za ajira kisekta na idadi kubwa zaidi ya ajira serikalini zimepatikana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iliyoajiri wafanyakazi 1,082 ikifuatiwa na Wizara ya Afya iliyoajiri wafanyakazi 725 katika kipindi hicho cha miaka minne.

Mhe. Spika, Mashirika ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi hicho cha miaka minne yaliweza kutoa na kuajiri nafasi 511 zilizohusisha wanaume 368 na wanawake 143. Halmashauri za Wilaya zimetoa na kuajiri jumla ya nafasi 84 za ajira zilizohusisha wanaume 50 na wanawake 34. Aidha, Serikali pia imeajiri jumla ya wafanyakazi 1,025 kwa misingi ya mikataba ya muda katika miradi mbali mbali iliyohusisha wanawake 595 na wanaume 340.

Mhe. Spika, kwa upande wa ajira katika sekta binafsi, jumla ya ajira 7,488 zimezalishwa katika kipindi cha miaka minne kutoka mwaka 2011/12 hadi 2014/15. Katika ajira hizo jumla ya ajira 5,024 sawa na asilimia 67.1 zimejazwa na wanaume na 2,464 sawa na asilimia 32.9 zimejazwa na wanawake. Taarifa zinaonyesha kwamba uajiri katika vikundi vya Ushirika na Uzalishaji (*SACCOS*) katika kipindi cha miaka mitatu kutoka mwaka 2012/13 hadi mwaka 2014/15 zimefikia 6,835 zilizotolewa kutoka vikundi 215 vya *SACCOS*. Idadi kubwa ya ajira hizo zimepatikana mwaka 2014/15 zilizofikia 3,246 sawa na asilimia 47.5 ikifuatiwa na ajira 2,164 sawa na asilimia 31.7 zilizopatikana katika mwaka 2013/14. Idadi ndogo ya nafasi hizo za ajira kutoka *SACCOS* ni 1,425 zilizopatikana katika mwaka 2012/13.

Mhe. Spika, Serikali pia katika kipindi hicho imeendelea kuratibu ajira za Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi ambapo jumla ya ajira 4,226 zilipatikana zilizohusisha wanaume 3,047 sawa na asilimia 72.1 na ajira 1,179 sawa na asilimia 27.9 kwa wanawake. Ajira hizi nyingi za Wazanzibari nje ya nchi zimepatikana katika nchi za Falme za Kiarabu kutokana na uhusiano mzuri uliopo kati ya Zanzibar na nchi hizi.

Mhe. Spika, Serikali itaendelea kuongeza juhudi zaidi kupitia utekelezaji wa mipango yake mikuu ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020 na MKUZA II ili kujenga mazingira yatakayotoa ajira zaidi hususan kwa vijana serikalini na sekta binafsi ili pamoja na mambo mengine kupunguza tatizo la ajira na kuwatumia vijana kama fursa badala ya kikwazo katika uzalishaji na maendeleo.

### vi) Mipango Endelevu ya Maendeleo ya Ardhi

Mhe. Spika, mipango mizuri na endelevu ya maendeleo lazima ioanishe mahitaji ya aina tatu; kijamii, kiuchumi na kimazingira. Mahitaji ya kimazingira yanaangaliwa katika kuhifadhi mazingira yenyewe, lakini yanaangaliwa vile vile katika kuweka mipango au mikakati imara ya matumizi bora ya ardhi na maendeleo mazuri ya miji. Kwa muda mrefu Zanzibar ilikuwa na vigezo visivyojitosheleza vya matumizi ya ardhi na maendeleo ya miji, kwa sababu mikakati ya matumizi ya ardhi na mipango ya miji ilipitwa na wakati. MKUZA II iliagiza sekta husika kuifanyia mapitio mipango ya matumizi ya ardhi.

Mhe. Spika, jitihada za Serikali zimefanikiwa katika kuondoa kasoro hii. Serikali iliridhia na kupitisha Mkakati wa Maendeleo ya Ardhi Zanzibar (*National Spatial Development Strategy – NSDS*) na Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Mji wa Zanzibar (*Master Plan of Zanzibar City).* Kazi hizi zimeweka miongozo imara na ya muda mrefu ya maendeleo ya ardhi Zanzibar inayozingatia mahitaji ya kukuza uchumi, kuweka maslahi ya kijamii, kutunza athari zake za kiutamaduni na kuhuisha miji yake. Hili linaifanya Zanzibar kuwa mstari wa mbele katika kujitayarisha kutekeleza viashiria vya kufikia malengo ya DIRA ya Maendeleo ya 2020 na vile vya maendeleo endelevu.

Aidha, mipango bora ya matumizi ya ardhi, Mahkama ya Ardhi na Usajili wa Ardhi inaendelea kuimarishwa ili kuondosha migogoro na kutenga ardhi kwa matumizi maalum kama vile ardhi kwa maeneo ya kilimo, ardhi ya uwekezaji na kwa ajili ya vianzio vya maji. Hayo yote ni mambo muhimu kwa maslahi ya Taifa na jamii. Utoaji wa ardhi *(land allocation*) kwa shughuli za kiuchumi na kijamii unapokuwa wa uhakika unaongeza nguvu ya ushindani wa kibiashara.

**vii) Utawala Bora**

Mhe. Spika, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita 2010/2011-2014/15 mafanikio ya utekelezaji yalitambua na kuthamini utawala bora. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya juhudi na kuchukua hatua mbali mbali ili kuhakikisha utawala bora unatekelezwa kwa kuzingatia misingi yake. Hatua hizo zilihusisha kufanya mageuzi ya kiutawala ambayo yamewezesha kuweka mazingira ya utekelezaji mzuri wa sera na miongozo mbali mbali ili kuimarisha utoaji huduma na ukuaji wa uchumi.

Aidha, serikali ilitayarisha muongozo wa haki za binadamu ambao umeandikwa kwa nukta nundu (*brail*) kwa ajili ya watu wenye ulemavu, Sera ya Utawala Bora imeandaliwa mwaka 2011 na kuanza kutumika. Sheria ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi ya mwaka 2012 imetayarishwa na imeanza kazi. Pia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma imetayarishwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi mwaka 2015.

Vile vile, Programu ya Elimu ya Uraia imeandaliwa kwa ajili ya utoaji wa elimu kwa njia ya redio, televisheni na elimu kwa wana vijiji ili kuwashirikisha wananchi na kamati za shehia, taasisi na watu binafsi na elimu ya haki za binadamu imetolewa katika Shehia mbali mbali za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, sasa naomba niwasilishe Mapitio ya Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2014/2015.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe naona minong'ono imekuwa, kiasi cha kwamba Waziri simsikii vizuri, nadhani na nyinyi inakuwa tabu kidogo kufuatilia kile anachokiwasilisha, naomba minong'ono iwe ya chini sana ili tusikie na tuweze kuzingatia kile kinachowasilishwa. Mhe. Waziri endelea.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora:**

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU/MIRADI YA MAENDELEO 2014/2015**

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/15 ulilenga kutekeleza jumla ya programu 32 na miradi 57 ya maendeleo kupitia klasta tatu za MKUZA II ambapo programu tatu ni mpya (zilizotokana na Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (*R4P)* unaojumuisha Programu Mjumuisho ya Kuimarisha Utalii, Programu ya Mazingira Bora ya Biashara na Programu ya Utafutaji Rasilimali Fedha) na miradi sita ni mipya.

Kwa mwaka 2014/2015, Programu na Miradi ya Maendeleo ilipangiwa jumla ya Shilingi 331.3 bilioni. Kati ya fedha hizo, Shilingi 65.9 bilioni zilitarajiwa kutolewa na Serikali na Shilingi 265.4 bilioni zilitarajiwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo Shilingi 66.3 bilioni ni ruzuku na Shilingi 199.1 bilioni ni mikopo.

Mhe. Spika, kufikia Machi 2015, jumla ya Shilingi 117.3 bilioni zilitolewa sawa na asilimia 35 ya bajeti ya maendeleo, ambapo Shilingi 39.1 bilioni zilitolewa na serikali sawa na asilimia 59 na Shilingi 78.2 bilioni sawa na asilimia 29 zilitolewa na Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, upatikanaji wa kiwango hiki cha fedha kwa miezi tisa kwa mwaka 2014/2015 ni upungufu wa Shilingi 12.4 bilioni sawa na asilimia 9.5 ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa 2013/2014 katika kipindi kama hicho ambapo Shilingi 129.7 bilioni zilipatikana. Kwa upande mwengine, kiwango hiki cha fedha ni asilimia 35 kwa miezi tisa kwa mwaka 2014/2015 ikilinganishwa na asilimia 42.5 kwa miezi tisa mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, serikali imeendelea kutekeleza azma ya kupunguza wingi wa miradi ili kuleta ufanisi wa utekelezaji kwa kukamilisha programu na miradi mitano, kupendekeza miradi itakayokamilika endapo ikiingiziwa fedha ili ikamilike mwaka huu na kuainisha miradi yenye uasili wa kazi za kawaida kuhamishwa kutoka kazi za maendeleo kama ifuatavyo:

A. Programu/Miradi iliyokamilika kwa mwaka 2014/2015 ni mitano nayo ni:

i) Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Ardhi (*SMOLE*);
ii) Mradi wa Utafiti wa Watenda kazi;
iii) Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya Pili;
iv) Ujenzi wa njia za kupitia ndege (*taxi ways*) uwanja wa ndege – Unguja;
v) Kupambana na Ajira mbaya - Zanzibar.

B. Miradi inayopendekezwa kukamilika mwaka 2014/15 ni 13 yenye jumla ya Shilingi 8.7 bilioni. Fedha hizi zikiingizwa miradi hii itakamilika.

C. Miradi inayopendekezwa kuhamishiwa katika kazi za kawaida ni mitano yenye jumla ya Shilingi 0.7 bilioni kwa bajeti ya mwaka 2014/15. Miradi hiyo ni:

i) Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu katika Afya ya Uzazi, Jinsia na Kupunguza Umasikini;
ii) Uhakika wa Chakula na Lishe;
iii) Kudhibiti Maradhi ya Mifugo yasiyokuwa na Mipaka (*TADs*);
iv) Uimarishaji wa Serikali za Mitaa;
v) Uimarishaji wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Spika, miradi hii inapendekezwa kuondolewa katika kazi za maendeleo kutokana na kuwa ni ya siku nyingi na haina muda wa kumalizika, kukosa vigezo vya kuwa mradi na kazi zake nyingi ni za kawaida (*routine*) kwa kila siku.

## UTEKELEZAJI WA MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2014/15

Katika mwaka 2014/15 SMZ iliendelea na juhudi za kukuza uchumi kwa kufanya mageuzi ya kiuchumi ili kufikia malengo ya MKUZA II na ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020. Mkazo uliwekwa katika utekelezaji wa Mpango wa Matokeo kwa Ustawi; utafiti; miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege pamoja na huduma za makundi maalum. Utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele ni kama ifuatavyo:

### Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (*R4P*)

Mhe. Spika, Katika kutekeleza maeneo yaliyoibuliwa kupitia Mpango wa Matokeo kwa Ustawi, Programu Mjumuisho ya Kuendeleza Utalii imeanza kwa ukaguzi wa visiwa 13 visivyokuwa na makaazi ya kudumu na kupendekezwa visiwa vinane kuwekezwa miradi ya utalii. Visiwa hivyo ni Pungume, Kwale, Niamembe, Miwi

na Vundwe kwa upande wa Unguja na Mtangani, Njiauze na Mbale kwa upande wa Pemba.

Kwa upande wa michezo ya baharini maeneo kadhaa yamekaguliwa na kupendekezwa maeneo manane (Unguja manne yakiwemo Mangapwani, Mchangamle, Kiwengwa na Pwanimchangani na Pemba manne pia yakiwemo Wambaa, Verani Mkunguni, Vumawimbi na Kiuyu Mbuyuni). Pia kuanzishwa Michezo ya Baharini ambapo Maandiko ya dhana ya miradi yameshatayarishwa. Mpango Mkakati wa Masoko umeanza utekelezaji wake, pamoja na kuanza matayarisho ya "*branding*" ya utalii na tovuti ya Taifa ya Utalii.

Aidha, michoro na uchambuzi wa shughuli, vifaa na gharama za ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya utoaji habari za utalii ngazi ya Wilaya imekamilika na rasimu ya utafiti wa Mahitaji ya Soko la Ajira la Utalii Unguja na Pemba imetayarishwa na kujadiliwa katika ngazi mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa upande wa Programu ya Kuimarisha Biashara, Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi wa Zanzibar umeshaidhinishwa na serikali. Mapitio ya Sera ya Biashara na Sera ya Maendeleo ya Ujasiriamali yameanza kwa kukusanya taarifa ambapo dhana za awali na hadidu rejea zimeshaandaliwa na rasimu ya awali ya mapendekezo ya kuandaa Sheria ya Maendeleo ya Wajasiriamali imekamilika. Ripoti ya awali ya maendeleo ya viwanda vidogo vidogo na vya kati nayo pia imekamilika.

Mhe. Spika, katika Programu ya Kuimarisha Upatikanaji wa Rasilimali Fedha, kwa upande wa kuimarisha mapato yasiyotokana na kodi, Mashirika ya Serikali yameanza kuchangia mapato na tayari Shilingi 727 milioni zimepatikana kwa kipindi cha miezi tisa.

Kuhusu kuimarisha mapato yatokanayo na kodi, serikali imepeleka maofisa wake kujifunza Tanzania Bara kuhusu matumizi ya mashine za risiti (*EFD*) na pia aina za mashine hizo zimeshapatikana na matayarisho ya ununuzi yameanza. Aidha, kuhusu Msimamizi wa Wahasibu na Wakaguzi wa hesabu, matayarisho ya sheria yameanza na vikao vya wadau vimefanyika.

**Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (*R4P*)**

Mhe. Spika, Katika kutekeleza maeneo yaliyoibuliwa kupitia Mpango wa Matokeo kwa Ustawi, Programu Mjumuisho ya Kuendeleza Utalii imeanza kwa ukaguzi wa visiwa 13 visivyokuwa na makaazi ya kudumu na kupendekezwa visiwa vinane kuwekezwa miradi ya utalii. Visiwa hivyo ni Pungume, Kwale, Niamembe, Miwi

na Vundwe kwa upande wa Unguja na Mtangani, Njiauze na Mbale kwa upande wa Pemba.

Kwa upande wa michezo ya baharini maeneo kadhaa yamekaguliwa na kupendekezwa maeneo manane (Unguja manne yakiwemo Mangapwani, Mchangamle, Kiwengwa na Pwanimchangani na Pemba manne pia yakiwemo Wambaa, Verani Mkunguni, Vumawimbi na Kiuyu Mbuyuni). Pia kuanzishwa Michezo ya Baharini ambapo Maandiko ya dhana ya miradi yameshatayarishwa. Mpango Mkakati wa Masoko umeanza utekelezaji wake, pamoja na kuanza matayarisho ya "*branding*" ya utalii na tovuti ya Taifa ya Utalii.

Aidha, michoro na uchambuzi wa shughuli, vifaa na gharama za ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya utoaji habari za utalii ngazi ya Wilaya imekamilika na rasimu ya utafiti wa Mahitaji ya Soko la Ajira la Utalii Unguja na Pemba imetayarishwa na kujadiliwa katika ngazi mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa upande wa Programu ya Kuimarisha Biashara, Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi wa Zanzibar umeshaidhinishwa na serikali. Mapitio ya Sera ya Biashara na Sera ya Maendeleo ya Ujasiriamali yameanza kwa kukusanya taarifa ambapo dhana za awali na hadidu rejea zimeshaandaliwa na rasimu ya awali ya mapendekezo ya kuandaa Sheria ya Maendeleo ya Wajasiriamali imekamilika. Ripoti ya awali ya maendeleo ya viwanda vidogo vidogo na vya kati nayo pia imekamilika.

Mhe. Spika, katika Programu ya Kuimarisha Upatikanaji wa Rasilimali Fedha, kwa upande wa kuimarisha mapato yasiyotokana na kodi, Mashirika ya Serikali yameanza kuchangia mapato na tayari Shilingi 727 milioni zimepatikana kwa kipindi cha miezi tisa.

Kuhusu kuimarisha mapato yatokanayo na kodi, serikali imepeleka maofisa wake kujifunza Tanzania Bara kuhusu matumizi ya mashine za risiti (*EFD*) na pia aina za mashine hizo zimeshapatikana na matayarisho ya ununuzi yameanza. Aidha, kuhusu Msimamizi wa Wahasibu na Wakaguzi wa hesabu, matayarisho ya sheria yameanza na vikao vya wadau vimefanyika.

Mhe. Spika, Kuhusu *PPP*, Sera ya Mashirikiano ya Sekta ya Umma na Binafsi (*PPP*) imethibitishwa na Sheria ya *PPP* imeshapitishwa na Baraza la Wawakilishi. Kitengo cha *PPP* kinaendelea kuimarishwa kwa watendaji wake kupatiwa mafunzo mbali mbali ndani na nje ya nchi. Aidha, washiriki wengine kutoka sekta za umma na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepatiwa mafunzo na semina kuhusiana na dhana nzima ya *PPP*, sera na sheria ya *PPP*.

**Kufanya tafiti katika sekta zote**

Mhe. Spika, Matayarisho ya ufanyaji tafiti za kitaifa yameanza ambapo Rasimu ya Muongozo wa Utafiti umeandaliwa na unatarajiwa kuwasilishwa katika Kikao cha Makatibu Wakuu kwa kupata maoni zaidi. Aidha, maeneo ya utafiti kitaifa yameibuliwa kulingana na vipaumbele vya kitaifa pamoja na kufanyika mafunzo ya utafiti kwa maafisa watatu nje ya nchi.

**Kuimarisha miundombinu hasa ya usafiri wa baharini, nchi kavu na anga**

Mhe. Spika, katika kupunguza tatizo la usafiri wa baharini, mchakato wa ununuzi wa meli mpya yenye kubeba abiria 1,200 na mizigo tani 200 upo katika hatua za mwisho, baada ya kukamilika kwa hatua za awali zikiwemo ukataji wa vyuma, uwekaji wa mkuku na kushushwa kwenye maji. Meli inatarajiwa kuondoka Korea ya Kusini mwishoni mwa mwezi Mei na kusafiri hadi Zanzibar ambapo inatarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi Juni 2015.

Aidha, ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 39 Unguja na Pemba umekamilika. Barabara hizo ni Wete-Konde (15 *km*), Wete-Gando (15 *km),* Amani-Mtoni (4.0 *km*) na Njianne-Umbuji (5.0 *km*). Aidha, barabara zenye urefu wa kilomita 17.3 zimefanyiwa matengenezo.

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya usafiri wa anga, ujenzi umefanyika wa njia za kupitia ndege na maegesho ya ndege, njia hizo zimeongezwa urefu kutoka mita 1,805 hadi kufikia mita 3,427. Eneo la maegesho ya ndege lenye ukubwa wa mita za mraba 48,000 pia limejengwa.

Mhe. Spika, kuhusu ujenzi wa jengo jipya la abiria, hatua zilizofikiwa hadi mwezi Machi 2015 ni ujenzi wa paa asilimia 48, ukuta wa nje asilimia 42, chumba cha genereta asilimia 35, upigaji wa plasta wa kuta za matofali asilimia 95, uwekaji wa miundombinu ya umeme, vipoza hewa na mabomba ya maji nao umefikia asilimia 35.Kuimarisha huduma za kijamii zikiwemo elimu bora, huduma za afya na upatikanaji wa maji safi na salama

Mhe. Spika, katika kuimarisha ubora wa elimu, ujenzi wa madarasa 180 na matengenezo ya skuli na madarasa mbali mbali yanaendelea kote Unguja na Pemba kwa kushirikiana na wadau, sambamba na ujenzi wa nyumba za walimu. Jumla ya walimu 25 wakiwemo 21 wa shahada ya kwanza kwa fani za sanaa, wawili wa fani ya sayansi na wawili wa stashahada ya ualimu ya sayansi wameajiriwa na kupangiwa kazi katika skuli mbali mbali za Unguja na Pemba sambamba na walimu 500 (300 Unguja na 200 Pemba) wa skuli 10 za sekondari

wa masomo ya sayansi. Pia wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kufundisha masomo ya sayansi.

Mhe. Spika, jitihada kubwa za kupunguza tatizo la vitabu na vikalio zinaendelea kuchukuliwa na serikali ambapo jumla ya vitabu 19,607 vimesambazwa katika maktaba za skuli 83 Unguja na Pemba. Pia uandishi wa vitabu vya masomo ya Sayansi, Sanaa na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano unaendelea vizuri. Aidha, madawati 1,245 na seti za meza na viti 1,109 vimesambazwa katika skuli za msingi Unguja na uchongaji wa madawati 2,245 na seti za viti na meza 2,078 kwa skuli za Pemba unaendelea vizuri kupitia fedha za kodi ya Bandari.

Mhe. Spika, wanafunzi 2,541 wapya na wanaoendelea katika vyuo mbali mbali vya nje na vile vya Tanzania Bara na wanaoendelea kwa vyuo vya Zanzibar wamepatiwa stahiki zao. Wanafunzi wapya 499 wakiwemo wanawake 114 na wanaume 385 wameandikishwa katika kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo. Ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala cha Wingwi Mtemani unaendelea vizuri ukiwepo katika hatua za mwisho ikiwemo sakafu, uunganishaji wa umeme na maji. Uandishi wa moduli 11 na miongozo 11 ya walimu wa kufundishia vituo vya Elimu Mbadala pia unaendelea. Aidha, marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Elimu Zanzibar yamefanyika kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na wadau mbali mbali.

Mhe. Spika, katika kuendeleza huduma za afya kwa uchunguzi na utibabu wa maradhi, Hospitali ya Mnazi Mmoja imepatiwa vifaa vipya kwa ajili ya uchunguzi wa maradhi ya mfumo wa chakula. Vifaa hivi vinawezesha kugundua na kutibu maradhi ya vidonda vya tumbo, uvimbe, saratani za mfumo wa chakula na mengineyo. Kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China huduma ya *ICU* imeimarishwa kwa kufanyiwa matengenezo wodi ya mifupa kuwa wodi ya wagonjwa wenye kuhitaji uangalizi wa karibu (*ICU*). Wodi hii mpya ya *ICU* yenye vitanda vinane imewekewa vifaa vya kisasa. Dawa na vifaa vyenye thamani ya Shilingi 3.97 bilioni vimepatikana pamoja na kuimarisha mfumo mpya wa uagiziaji wa dawa uitwao *'framework contract'* ambao utapunguza uhaba wa upatikanaji wa dawa badala ya kutegemea Bohari Kuu ya Dawa ya Dar es Salaam, sambamba na uanzishwaji wa mfumo mpya wa usambazaji wa dawa kwa kutumia elektroniki ambao utaimarisha upatikanaji sahihi wa dawa, vifaa na kumbukumbu za matumizi yake.

Mhe. Spika, katika kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya, ujenzi wa jengo la watoto ambalo litatoa huduma ya maradhi ya figo unaendelea vizuri, ujenzi wa jengo la huduma za mama na mtoto unatarajiwa kuanza baada ya kukamilika shughuli za uvunjaji wa ndani wa jengo la kiwanda cha zamani cha dawa na zabuni kwa ajili ya matengenezo ya jengo la huduma ya matibabu ya

macho inaendelea kukamilishwa. Aidha, ujenzi wa jengo la maradhi ya kichwa na uti wa mgongo umekamilika na tayari jengo limefunguliwa rasmi na kuanza kazi.

Mhe. Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama, kazi ya ununuzi na ulazaji wa mabomba ya maji na viungo vyake inaendelea katika maeneo mbali mbali mijini na vijijini, sambamba na ujenzi wa uzio katika eneo la chemchem ya Mwanyanya na Mtoni. Ujenzi wa matangi katika maeneo ya Mnara wa Mbao na Saateni pia unakwenda vizuri. Uchimbaji wa visima katika maeneo ya Masingini, Mtofaani, Michamvi, Kinduni na Kibuteni umekamilika.

Aidha, ununuzi na uwekaji wa pampu na mota mpya umefanyika kwa maeneo mbali mbali ya vijijini, Unguja na Pemba. Mafunzo kwa wafanyakazi yanaendelea kutolewa ndani na nje ya nchi ili kuimarisha uwezo wa taasisi katika ukusanyaji wa mapato na kudhibiti maji yanayopotea.

**Kuimarisha huduma kwa makundi maalum**

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za makundi maalum, jumla ya familia 148 ambapo Unguja 89 na Pemba 59 zenye watoto wanaoishi katika mazingira magumu zimepatiwa msaada wa kifedha na huduma nyengine muhimu. Vile vile watoto 27 wanaoishi katika nyumba ya kulelea watoto wamepatiwa huduma za msingi na kwa wakati. Hatua ya kuimarisha Mfumo Haki kwa watoto wanaokinzana na sheria (*Child Justice*) umeanza kwa mchakato wa kuanzisha nyumba za kuwarekebisha watoto pamoja na kuimarisha mfumo wa kukusanya taarifa za watoto wanaokinzana na sheria.

Mhe. Spika, vile vile katika kuhakikisha wazee wote wanaofikia umri wa miaka 70 na kuendelea wanapatiwa pencheni, ziara za matayarisho zimeshaanza kufanyika katika mikoa na wilaya za Unguja kwa kuonana na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watendaji wakiwemo Masheha ili kueleza nia ya serikali na kupanga vyema zoezi la kuwatambua na kuwasajili wazee wote wenye umri wa miaka 70 na kuendelea.

Zoezi hili linaendelea vizuri katika Wilaya ya Kaskazini “A” Unguja na kwa Pemba linatarajiwa kuanza mara baada ya kumalizika Wilaya ya Kaskazini “A”. Utoaji wa pencheni jamii kwa wazee wote wa umri unaoanzia miaka 70 unategemewa kuanza mara baada ya kukamilika kwa taratibu.

Aidha, katika kuimarisha huduma za makundi maalum, Sera ya watu wenye ulemavu imekamilika na rasimu ya Mpango Kazi wa Sera hiyo imeandaliwa. Visaidizi mbali mbali kwa watu wenye ulemavu vimetolewa pamoja na kufanyika mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Fedha kwa wajumbe wa Jumuiya za watu

wenye ulemavu sambamba na kufanyika ziara kwa wajumbe wa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu kwa taasisi mbali mbali za Serikali. Aidha, maadhimisho ya siku ya kimataifa kwa watu wenye ulemavu yamefanyika.

Mhe. Spika, Kupitia mradi wa *TASAF* malipo ya TZS 1.12 bilioni katika awamu mbali mbali yamefanyika kupitia mpango wa kunusuru kaya masikini katika shehia 40 (Unguja 20 na Pemba 20). Uzinduzi rasmi wa malipo ya kwanza ya kazi ya miradi ya kutoa ajira ya muda umefanyika katika shehia ya Muyuni "B" Unguja. Jumla ya miradi 77 imeendelea kutekelezwa na walengwa wa mpango wa kunusuru kaya masikini kwa Unguja na Pemba ambapo jumla ya TZS 649.1 milioni zimelipwa katika mwezi wa Januari na Februari mwaka 2015. Kwa Unguja TZS 228.2 milioni na Pemba TZS 420.9 milioni.

## MUELEKEO WA HALI YA UCHUMI 2015

### Muelekeo wa Uchumi wa Dunia

Mhe. Spika, Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), kasi ya ukuaji wa uchumi inatarajiwa kuongezeka kufikia asilimia 3.5 mwaka 2015. Uchumi wa nchi zilizoendelea nao unatarajiwa kukua kwa asilimia 2.4 kwa mwaka 2015. Hali hii ni kutokana na kurejea pole pole kwa hali nzuri ya uchumi wa nchi za Ulaya Magharibi na Japan pia kuongezeka kwa usafirishaji na kushuka kwa bei za vyakula na mafuta.

Mhe. Spika, Kwa upande mwengine uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kukua hadi kufikia asilimia 4.5 kwa mwaka 2015. Hali hii itatokana na kuimarika kwa uzalishaji katika sekta ya kilimo, kuongezeka kwa sekta ya huduma na kuimarika kwa uwekezaji endelevu wa miundombinu.

## MUELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR

Mhe. Spika, Utekelezaji wa malengo ya uchumi unatarajiwa kwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini awamu ya pili, Malengo ya Milenia baada ya 2015 pamoja na Mageuzi ya Msingi na Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2015 uchumi unatarajiwa kukua kwa kasi ndogo ya asilimia 6.8 kutoka asilimia 7.0 mwaka 2014. Matarajio ya ukuaji wa uchumi yanatokana na mambo yafuatayo:

i) Kuanza utekelezaji wa miradi ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

ii) Kuendelea kuimarika kwa miundombinu ya usafiri, umeme, maji na mawasiliano.
iii) Kuimarika kwa hali ya rasilimali watu.
iv) Kuimarika kwa mazingira ya afya na elimu.
v) Kuendelea kuimarisha amani na utulivu wa kisiasa pamoja na uwazi na uwajibikaji katika utendaji wetu.
vi) Kuendelea kuimarisha vyanzo vya kodi na elimu ya ulipaji kodi kwa hiyari; na
vii) Kuendelea kutekeleza Programu za Mpango wa Matokeo kwa ustawi.

Mhe. Spika, hata hivyo, uchumi wetu unatarajiwa kukua kwa kasi ndogo kwa mwaka 2015 kutokana na sababu zifuatazo:

i) Kwa kawaida katika mwaka wa uchaguzi mkuu idadi ya watalii wanaoingia nchini huwa inapungua.
ii) Kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya kimarekani.
iii) Msimu mdogo wa uzalishaji wa zao la Karafuu ambalo lina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi.
iv) Uwezekano wa kupungua kwa mvua kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.
v) Kuendelea kuagiza chakula kutoka nje ya Zanzibar kutokana na uzalishaji wetu mdogo wa mazao ya nafaka na mengineyo.
vi) Kujitokeza kwa maradhi ya migomba na wadudu waharibifu wa mihogo.

Mhe. Spika, Pamoja na matarajio ya kukua kwa kasi ndogo kwa uchumi wa Zanzibar, hali ya mfumko wa bei inatarajiwa kuwa tulivu na kuendelea kubakia katika tarakimu moja. Matarajio haya ni kutokana na matarajio ya kushuka kwa mfumko wa bei duniani pia kuimarika kwa sekta ya Uvuvi na Mifugo.

## MUELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2015/16

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2015/16, utajikita zaidi katika umaliziaji wa miradi inayoendelea na kuimarisha maeneo muhimu ya huduma za jamii. Mpango huo unalenga kutekeleza jumla ya programu 28 na miradi 37 ya maendeleo kupitia klasta tatu za MKUZA II ambapo miradi minne ni mipya.

## MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2015/16

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2015/2016, maeneo yatakayopewa kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ni kama yafuatayo:

i) Kutekeleza Programu Mjumuisho ya kuendeleza Utalii, Programu ya kuimarisha Mazingira ya Biashara na Mkakati wa utafutaji Rasilimali Fedha iliyoibuliwa katika Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (*Results for Prosperity – R4P*);

ii) Kuimarisha huduma za kijamii zikiwemo:

- elimu bora kwa kuondosha michango ya skuli za msingi, kuchonga madawati na ujenzi wa vituo viwili vya Elimu Mbadala na Amali;
- huduma za afya kwa kuendelea na ujenzi wa majengo ya mama na mtoto, ujenzi wa hospitali ya Abdalla Mzee na ununuzi wa dawa, vifaa na nyenzo nyengine;
- upatikanaji wa maji safi na salama kwa maeneo ya mijini na vijijini kwa uchimbaji wa visima, ulazaji wa mabomba na ujenzi wa matangi.

iii) Kuendeleza sekta ya Nishati na kuweka mifumo stahiki katika kuendeleza sekta ya mafuta na gesi kwa kutoa mafunzo na kuandaa vyombo vya kisheria;

iv) Kuendeleza shughuli za kukuza ajira kwa vijana. Mkazo ni kuwajengea uwezo wa kuajirika na kujiajiri kutokana na mambo yafuatayo :

- Kubadilisha mitazamo ya vijana kuhusu ajira, wasitegemee tu kazi za Serikali na badala yake watumie fursa zilizopo kujiajiri wenyewe;
- Kuwajengea vijana utamaduni na uwezo wa ujasiriamali ili watumie fursa zilizopo kujiajiri;
- Kuwapatia vijana huduma za uendelezaji biashara kupitia Kituo cha Kukuza Ujasiriamali;
- Kuwashajiisha na kuwawezesha vijana kujiajiri katika shughuli za kilimo kupitia vyama vya ushirika; na
- Kuwawezesha vijana kufanya shughuli za ujasiriamali kwa kuwapatia mikopo ya masharti nafuu kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

v) Kuendeleza uvuvi wa bahari kuu;

vi) Kuimarisha na kuendelea kuvutia wawekezaji kwa sekta ya viwanda na maeneo huru ya kiuchumi na miradi mikakati (*Strategic Investments*).

- Kwa upande wa viwanda kutayarisha vivutio kwa ajili ya kuvutia uwekezaji wa viwanda.
- kuendeleza majadiliano na utekelezaji wa miradi mikakati sita itakayoratibiwa na *ZIPA* ambayo ni kama ifuatavyo:

1. Uendelezaji wa mji wa kisasa wa biashara wa Fumba utakaohusisha *ZIPA* na *Bakhressa Group of Companies*;

2. Maendeleo ya Mji wa kisasa Kijini Matemwe pia kiwanja cha Golf na hoteli kupitia mradi wa *Penny Royal Real Estate*;
*3*. Kuendeleza hoteli ya Bwawani na eneo linaloambatana nalo kupitia Kampuni ya *Quality Group Limited;*
4. Kujenga kituo cha mikutano cha kimataifa Dimani;
5. Kuendeleza eneo la viwanda Fumba kupitia *CPC Egypt*;
6. Mradi wa kuendeleza mji wa Fumba kupitia *CPS Live*.

**MUELEKEO WA PROGRAMU/MIRADI KWA MWAKA 2015/2016**

Mhe. Spika, Programu na miradi mbali mbali itatekelezwa katika mwaka 2015/2016 kupitia klasta tatu za MKUZA.

i) **Klasta ya kwanza: Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato**:

Katika sekta ya kilimo, Serikali itaendelea kutekeleza programu ya miundombinu ya soko, kuongeza thamani ya mazao na misaada vijijini kwa kulipia fidia mazao na miti iliyoathirika kwa ajili ya ujengaji wa barabara, kununua na kufunga mitambo miwili ya kuzalisha barafu na kuendelea kutoa elimu ya upotevu wa mazao kwa kukarabati vituo vya Cheju na Ole.

Kwa programu ya kuendeleza sekta ya kilimo/mifugo, Serikali itaendelea kuvipatia taaluma vikundi vya wakulima 1,200 na kununua mbegu kwa ajili ya kupandishia ng'ombe. Aidha, itaendelea kufanya tafiti za mazao mbali mbali na kutoa mafunzo kwa watafiti.

Kwa programu ya umwagiliaji maji, Serikali itamalizia michoro na kuanza ujenzi katika maeneo ya Cheju, Kilombero, Kibokwa, Chaani, Kinyasini, Mlemele na Makwararani. Aidha, Serikali itaendeleza programu ya kusaidia kilimo na uhakika wa chakula na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo ya Kibonde Mzungu, Mtwango, Koani, Mchangani na Bandamaji kwa Unguja na Ole, Kwalempona, Machijini na Dobi kwa Pemba. Aidha, mradi wa kuimarisha mikarafuu utaendelea kwa kuzalisha miche 1,000,000 ya mikarafuu kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Kwa upande wa mifugo programu ya kuendeleza miundombinu ya ufugaji itaendelea kwa kujenga kituo cha huduma za utabibu na uzalishaji Makangale na Mbweni. Kwa upande wa uvuvi Serikali itaendeleza programu ya kuimarisha uvuvi kwa kutekeleza mradi wa kuimarisha mazao ya baharini na mradi wa kuendeleza uvuvi wa bahari kuu kwa kujenga soko na diko la samaki Malindi.

Mhe. Spika, Kwa upande wa nishati Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa sera ya nishati awamu ya pili kwa utayarishaji wa mpango mkuu wa matumizi bora ya nishati na kuendelea na uchambuzi yakinifu wa vyanzo vya nishati mbadala kwa usambazaji na ufungaji wa vifaa vya umeme wa upepo na jua katika maeneo matano yaliyoteuliwa. Vile vile Serikali kwa upande wa umeme vijijini itaendelea ujenzi wa laini kubwa na laini ndogo kwa maeneo ya vijijini.

Mhe. Spika, Kuhusu miundombinu, programu ya ujenzi wa barabara itaendeleza ujenzi wa barabara sita za vijijini zenye urefu wa kilomita 48.9 kwa maeneo ya Kichwele-Pangeni (4*km*), Matemwe - Muyuni (6.5*km*), Umbuji-Uroa (6.8 *km*), Fuoni-Kombeni (8.5 km), Jozani-Charawe-Ukongoroni-Bwejuu (22.7 *km*), Mkwajuni - Kijini (9.3*km*) na Pale -Kiongele (4.5*km*). Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara ya Ole-Kengeja. Vile vile itaendelea na programu ya kuimarisha viwanja vya ndege kwa kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la abiria na mradi wa huduma wa uwanja wa ndege wa Pemba. Kwa upande wa ujenzi wa bandari ya Mpigaduri, Serikali itaendelea na matayarisho wakati ikisubiri upatikanaji wa fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China baada ya kukamilika mradi wa ujenzi wa jengo jipya la abiria la uwanja wa ndege.

Mhe. Spika, Kuhusu sekta ya Fedha, Mipango, Utalii na Biashara, Serikali itaendelea na utekelezaji wa programu ya Upatikanaji wa Rasilimali Fedha na mradi wa Mageuzi ya Fedha za Umma. Vile vile, Serikali itaendelea kuimarisha huduma za miji kwa kuanza ujenzi wa michirizi ya maji ya mvua katika maeneo mbali mbali ya ng’ambo na kuweka taa za barabarani katika maeneo ya mji wa manispaa ya Zanzibar na kujenga ukuta wa kuzuia mmong’onyoko wa ardhi katika eneo la pembezoni mwa bahari hapo Mizingani. Vile vile Serikali itatekeleza mradi wa kujenga uwezo kwa kuratibu mapitio ya MKUZA II na maandalizi ya mkakati mpya. Pia programu ya MKURABITA itaendelea kwa kufanya usajili wa ardhi katika maeneo yaliyofanyiwa utambuzi wa ardhi ikiwemo Jang’ombe na Welezo kwa Unguja na Chokocho na Limbani kwa Pemba. Aidha Serikali itaendelea kuratibu utekelezaji wa programu mjumuisho ya maendeleo ya utalii na programu ya kuweka mazingira bora ya biashara. Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango utaendelea na ujenzi wa jengo la maabara.

ii) **Klasta ya pili: kuimarisha huduma na ustawi wa jamii*:***

Kwa upande wa elimu, Serikali itaendeleza mradi wa uimarishaji wa elimu za maandalizi kwa ujenzi wa skuli ya maandalizi ya Kajengwa na Chambani. Aidha, itaendeleza mradi wa uimarishaji wa elimu ya msingi kwa kuendelea kukamilisha ujenzi wa madarasa 500 yaliyoanzishwa na wananchi na pia itaendelea na kuimarisha elimu ya lazima kwa kukamilisha ujenzi wa skuli za sekondari ya

Kibuteni na Mkanyageni. Kwa upande wa mradi wa uimarishaji wa elimu mbadala na elimu ya amali kazi itaendelea ya ukarabati na utanuzi wa taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na Chuo cha Utalii Maruhubi.

Mhe. Spika, Kwa upande wa sekta ya afya Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya afya kwa kuendelea na kuipandisha hadhi hospitali ya Mnazimmoja kwa kuendelea na ujenzi wa wodi ya watoto, ukarabati ya Wodi ya Macho na jengo la *VIP*. Azma ya kupandisha hadhi hospitali za Wilaya inaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani Pemba umeanza vizuri. Vile vile Serikali itaendelea na Programu Shirikishi kwa kudhibiti maradhi ya ukimwi, kifua kikuu, ukoma na programu ya kudhibiti malaria.

Mhe. Spika, Kuhusu sekta ya maji, Serikali itaendelea kuhuisha maji mijini, kuimarisha miundombinu ya maji Mkoa wa Mjini Magharibi na usambazaji wa maji vijijini pamoja na kuendelea kujenga uwezo Mamlaka ya Maji awamu ya pili. Kwa upande wa michezo Serikali tayari imeshakamilisha makubaliano na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kuanza kazi ya mradi wa ukarabati wa kiwanja cha michezo cha Mao dze Tong.

iii) **Klasta ya tatu: Utawala bora na umoja wa kitaifa:** Mhe. Spika, kazi itaendelea na kutekeleza mradi wa kuimarisha nyumba za viongozi na nyumba za Serikali, mradi wa ujenzi wa chelezo cha uokozi na mradi wa mji salama kwa kufunga mitambo na vifaa katika maeneo yatakayoteuliwa. Aidha, programu ya *TASAF* itaendelea kwa kuibua kaya maskini katika Shehia 58 na uhaulishaji wa fedha wa kaya maskini na mradi wa kujenga uwezo wa kukabiliana na maafa. Pia, programu ya mabadiliko katika sekta ya sheria itatekelezwa pamoja na mradi wa usajili wa biashara. Vile vile, mradi wa Uimarishaji wa Takwimu utaendelea kwa kupewa uzito unaostahiki, hasa ukizingatia kwamba takwimu ni nyenzo muhimu katika kuandaa mipango ya maendeleo ya nchi.

**RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2015/16**

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2015/16 unalenga kutekeleza programu na miradi ya maendeleo kupitia klasta tatu za *MKUZA II* yenye jumla ya TZS 399.0 bilioni kwa ajili ya kugharamia programu na miradi mbali mbali ya maendeleo. Serikali itatoa TZS 51.9 bilioni sawa na asilimia 13 ya bajeti yote ya maendeleo ambapo kati ya hizo, TZS 39.1 bilioni ni kwa miradi ya vipaumbele, yenye mikataba au dhima kubwa kwa nchi na TZS 12.8 bilioni kwa miradi mengine. Aidha, TZS 347.1 bilioni sawa na asilimia 87 zitatolewa na Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS 98.2 bilioni ni ruzuku na TZS 248.9 bilioni ni mkopo.

1. Mhe. Spika, katika kutayarisha makisio ya kugharamia wa Mpango wa Maendeleo kutoka katika fedha za ndani, masuala yafuatayo yamezingatiwa:

a) Programu na miradi inayotokana na Mpango wa Matokeo kwa Ustawi inapewa kipaumbele;

b) Mgao wa rasilimali kwa mwaka 2015/16 utazingatia miradi inayoendelea kwa kutoa kipaumbele kwa miradi inayotarajiwa kumalizika 2015/16;

c) Madai yanayotokana na wakandarasi na watoa huduma wengine;

d) Miradi yenye uasili wa kazi za kawaida kuondoshwa katika bajeti ya maendeleo na kazi zake kuwekwa katika bajeti ya kawaida.

**UFUATILIAJI NA TATHMINI YA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO**

Mhe. Spika, Tume ya Mipango imeendelea kufanya ziara za ufuatiliaji wa programu na miradi ya maendeleo yenye kutekelezwa katika bajeti ya Serikali kupitia sekta mbali mbali. Katika mwaka 2014/15 ziara mbili zimefanywa ambapo programu 22 na miradi 46 ya maendeleo yenye kutekelezwa Unguja na Pemba ilitembelewa. Lengo la ziara hizo ni kuangalia utekelezaji halisi wa programu/miradi ya maendeleo sambamba na kuendelea na zoezi la upunguzaji wa programu/miradi ili kuwa na miradi michache yenye kutekelezeka na kuleta tija zaidi.

Mhe. Spika, Tathmini ya ziara hizo inaonesha mapungufu mbali mbali katika kutekeleza miradi ikiwemo baadhi ya miradi kuwa na bajeti kubwa na upatikanaji wa fedha za kutekelezea kuwa mdogo, na baadhi ya miradi kutekeleza shughuli za kawaida za sekta. Aidha baadhi ya miradi ina muda mrefu wa utekelezaji hivyo inashindwa kupima matokeo yaliyopangwa.

Changamoto nyengine katika utekelezaji wa programu na miradi ni uhaba wa upatikanaji wa fedha unaosababisha baadhi ya kazi kutokamilika kwa wakati uliopangwa; na baadhi ya miradi kutofanyiwa uchambuzi yakinifu kabla ya kuanzishwa.

Mhe. Spika, Katika kukabiliana na changamoto hizo, hatua mbali mbali zimependekezwa kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo. Hatua hizi ni pamoja na hizi zifuatazo:

i) Programu/miradi yote isiyo na sifa za kimradi ihamishiwe katika kazi za kawaida;

ii) Programu/miradi yenye utekelezaji wa muda mrefu igaiwe kwa awamu ili iweze kupima matokeo yake;

iii) Programu/miradi yote inayotarajiwa kukamilika kwa mwaka 2014/15 ipatiwe fedha zake zote zilizopangwa ili kukamilisha kazi zake kwa wakati;
iv) Kazi za ukarabati wa majengo zihamishiwe katika matumizi ya kawaida.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka 2015/2016 Serikali itaendelea kutumia Mpango wa Ufuatiliaji wa MKUZA na Mfumo wa Uwajibikaji wa MKUZA katika kutayarisha Mapitio ya MKUZA II na kufuatilia utekelezaji wa Programu na Miradi ya maendeleo iliomo katika mpango. Kuendelea kuratibu vikao vya kila robo mwaka kwa waratibu wa mpango wa matokeo kwa ustawi.

## HITIMISHO

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kukusanya mapato kwa ufanisi ili yaweze kupangwa vizuri katika matumizi, ikiwemo utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo. Ingawa bado tuna changamoto ya idadi ya watu Zanzibar, kuna haja kubwa ya kusimamia mipango yetu ili iweze kuleta tija na kuwanufaisha wananchi wetu. Jukumu hili la kusimamia ni letu sote.

Aidha, amani na utulivu katika nchi yetu ndio msingi imara wa kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu. Kwani dhima ya wananchi ni yetu sote. Hivyo wakati huu tunaelekea katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015, naomba kutoa wito kwa viongozi wenzangu na wananchi kwa jumla tuilinde amani tuliyonayo, na nachukua fursa hii kwa mara nyengine tena kuwatakia wananchi wote uchaguzi wa salama. (*Makofi*)

Mhe. Spika, umaliziaji wa hotuba yangu hii usingeweza kukamilika bila ya shukurani za kipekee kwa watendaji wote wa Tume ya Mipango wakiongozwa na Katibu Mtendaji Bibi Amina Khamis Shaaban, Kamishna wa Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini, Kamishna wa Ukuzaji Uchumi na Kamishna wa Maendeleo ya Watendakazi kwa kusimamia kwa umahiri kazi za kila siku za Tume ya Mipango na maandalizi ya hotuba hii.

Pia natoa shukurani kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali na watendaji wake wote kwa kutupatia takwimu kwa ajili ya matayarisho ya hotuba hii. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba pia kumshukuru Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu Ndugu Khamis Mussa Omar na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na Tume ya Mipango. Aidha, natoa shukrani kwa Makatibu Wakuu wa Wizara zote za SMZ na Watendaji wao kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika mchakato mzima wa matayarisho ya hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo. Ni matumaini yangu kwamba tutashirikiana zaidi katika utekelezaji katika siku zijazo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Kwa aina ya kipekee naomba kuyashukuru Mashirika ya Kimataifa na Nchi Wahisani kwa misaada ya kifedha na kiutaalamu wanaoendelea kutupatia wakiwemo ADB, ACRA, BADEA, BELGIUM, CARE AUSTRIA, CDC, CHAI, CHINA, CANADA, CIDA, DANIDA, EAC, EGH, EGYPT, EU, EXIM BANK, FAO, FINLAND, GAVI, GEF, GERMANY, GLOBAL FUND, GRFC, GPE, INDIA, ICAP, IFAD, ILO, IMF, OPEC, ITC, JAPAN, JICA, MCC, MILELE FOUNDATION, NMB, NORWAY, OFID, ORIO - Nertherland, KOREA, SAUDI FUND, Save the Children, SIDA, SWEDEN, OMAN, UK, UTURUKI, UNDP, UNESCO, UNFPA, UNICEF, UNIDO, URT, USA, USAID, UN-HABITAT, UN WOMEN, WB, WHO, WIPO, na WSPA. Vile vile kama kuna nchi na taasisi yoyote kwa bahati mbaya tuliyoisahau wote tunawashukuru. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Dimani kwa kuendelea kunisaidia na kunipa ushirikiano mkubwa katika kazi zangu za Jimbo. Nawashukuru pia kwa ufahamu wao na ustahamilivu wao kwa baadhi ya nyakati wakinihitajia lakini hawakunipata kwa utekelezaji wa majukumu ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba sasa Baraza lako Tukufu, lipokee, lijadili na kupitisha mapendekezo ya Muelekeo wa Uchumi mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kwa kuwasilisha. Nakushukuru kwa kuwasilisha hotuba hiyo juu ya hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka 2015/2016 na hoja hiyo Waheshimiwa Wajumbe mumeiunga mkono.

Utaratibu wetu ni kwamba mjadala wa hoja hii pamoja na mjadala wa Bajeti ya Serikali vitajadiliwa kwa pamoja Mwenyezi Mungu akitujaalia siku wa Jumatatu.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru tupitishe sasa utaratibu kuhusu kikao cha jioni. Kikao cha kusoma Bajeti ya Serikali, Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli zilizopangwa kwa asubuhi hii zimekamilika, na kwa kuwa leo jioni tutakuwa na Bajeti ya Serikali itakayosomwa saa 10:00 kutoka na utamaduni wetu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba kutoa hoja ili Baraza lako Tukufu liweke kanuni

ya muda kando ili tuakhirishe kwa sasa na tuweze kukutana tena jioni hii leo saa 10:00 barabara ili kusikiliza Hotuba ya Bajeti itakayotolewa na Mhe. Waziri wa Fedha. Mhe. Spika naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Waheshimiwa, basi niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe sasa leo ni siku ya hotuba ya Bajeti ya Serikali na kama tulivyoamua sasa kwamba shughuli ya kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali itafanyika saa 10: 00 jioni badala ya utaratibu wa kawaida ya kuja saa 11:00. Niombe basi Waheshimiwa Wajumbe tuwe tunawahi mapema tutakuwa na wageni tumewaalika sasa isiwe wageni wanafika mapema zaidi kuliko sisi wenyewe.

Nategemea Waheshimwia Wajumbe wote tuwemo humu ndani kuanzia saa 9:30 pamoja na wageni wetu watafika mapema kama tulivyowaalika ili saa 10:00 barabara tumkaribishe Waziri wa Fedha na mkoba wake wa Bajeti ya Serikali, jana amenambia umenona vizuri sana ili awasilishe mkoba huo kwenye ukumbi wetu wetu huu wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa kuwa shughuli zilizopangwa kwa leo tumefikia tamati, naomba sasa tuakhirishe kikao hiki hadi saa 10:00 jioni leo.

*(Saa 5: 28 Asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi zaa 10:00 jioni)*

*(Saa 10:00 jioni Baraza lilirudia)*

**Mhe. Spika:** Wajumbe kama tulivyopeana taarifa mapema pale asubuhi, kwamba leo ni siku ya bajeti na kwa utamaduni wetu Waziri wa Fedha amejificha pahala na mkoba wake wa bajeti, sasa ninamuamuru *sergeant at arms* akamtafute amlete atusomee bajeti yetu ya mwaka 2015/2016, bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *Sergeant at arms* kamtafute Waziri wa Fedha umlete. Amejificha mbali kidogo, lakini naona dalili sasa analetwa, yule.

*(Hapa Sergeant at arms alitoka nje kumtafuta Waziri wa Fedha na kuingia naye)*

**Mhe. Spika:** Sasa Mhe. Waziri wa Fedha anaingia. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Fedha karibu sana utuwasilishie bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2015/2016, karibu sana Mhe. Waziri.

**Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/16**

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika**,** kama ilivyo ada kwetu sisi waumini, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu muumba wa mbingu na ardhi kwa kutujaalia neema ya uhai na afya zilizotuwezesha kukutana hapa. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2015/16, ili kutimiza matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kama ilivyorekebishwa.

Mhe. Spika**,** leo asubuhi Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora amewasilisha mbele ya Baraza hili Taarifa ya Mwenendo na Hali ya Uchumi wa Zanzibar, Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/15 kwa kipindi cha miezi tisa hadi Machi mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2015/16. Makadirio ya mapato na matumizi ninayowasilisha yanakamilisha mustakabali wetu kiuchumi, kimaendeleo na kifedha kwa upande wa mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Mhe. Spika, naomba hotuba hii, isomwe sambamba na Rasimu ya Mapendekezo ya Mapato na Matumizi na kuingizwa kwenye kumbukumbu za Baraza.

Mhe. Spika, naomba pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumaliza mwaka mwengine wa uongozi wake kwa nchi yetu. Tumeshuhudia katika mwaka huu kwa mara nyengine tena, uongozi wake ulio bora, imara na wa uadilifu mkubwa. Nawapongeza pia wasaidizi wake wakuu, Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais, kwa ushauri na msaada wao kwa Mhe. Rais.

Sina budi pia kumshukuru sana Mhe. Rais kwa kuendelea kuniamini na kunikabidhi jukumu la kuiongoza Wizara ya Fedha, wizara ambayo ina umuhimu wa kipekee kwa maendeleo ya nchi yetu. Nawashukuru viongozi hawa wote kwa miongozo yao ya kila mara inayonirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nimkumbuke mwenzetu ambaye tumekuwa naye katika hotuba zote za Bajeti kwa miaka minne iliyopita na kupata mchango wake adhimu lakini mara hii hatunaye tena. Ninamuomba tena

Mwenyezi Mungu, Subhana Wataala, kumpa malazi mema mpenzi wetu, ndugu yetu na mwenzetu, Marehemu Salmin Awadh Salmin aliyetangulia mbele ya haki tarehe 19 Februari 2015. Ninamuomba pia amlipe vyema kwa mchango wake mkubwa alioutoa kwa maendeleo ya wanajamii wenzake na ajaalie mchango huo uwe sadaka yake inayoendelea.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nianze kwa kuzungumzia kwa ufupi hali ya uchumi wetu.

## B. MWENENDO WA UCHUMI WA ZANZIBAR

Mhe. Spika; kama nilivyosema awali, tayari asubuhi ya leo tumewasilishiwa matokeo ya mwenendo wa uchumi wetu kwa mwaka 2014 na matarajio kwa mwaka 2015. Taarifa hiyo imeeleza kuwa Uchumi wa Zanzibar umeendelea kukua kwa kiwango kizuri pamoja na kuendelea kuwepo kwa utulivu wa bei za bidhaa na huduma.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014 taarifa imeonesha kuwa uchumi wetu umekuwa kwa asilimia 7.0 ikionesha kupungua kidogo kwa kasi yake ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.2 kwa mwaka 2013. Kwa mafanikio hayo, wastani wa Pato la Taifa la kila mtu limeongezeka na sasa limefikia TZS 1,552,000 sawa na Dola za Kimarekani 939 mwaka 2014 kutoka TZS 1,384,000 sawa na Dola za Kimarekani 866 kwa mwaka 2013.

Mhe. Spika, kimuundo, uchumi wetu umeendelea kuchangiwa zaidi na Sekta ya Huduma ikifuatiwa na Kilimo. Kwa mwaka 2014, Sekta ya Huduma ilichangia asilimia 44.7, ikionesha kupanda kwa mchango wake kutoka asilimia 41.5 wa mwaka 2013. Hali hii imetokana na kuimarika kwa Sekta ndogo za Habari na Mawasiliano; Fedha na Taaluma, Ufundi na Sayansi.

Mchango wa sekta ya Kilimo kwa mwaka 2014 umepungua na kufikia asilimia 27.9 kutoka asilimia 30.4 mwaka 2013 kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa mpunga na mazao mengine ya chakula pamoja na kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya biashara, hasa karafuu. Halikadhalika, mafanikio mazuri ya Sekta ya Huduma yameshusha pia mchango wa Sekta ya Viwanda kutoka asilimia 18.0 mwaka 2013 hadi kufikia asilimia 16.8 mwaka 2014. Hali hii imetokana na kushuka kwa mchango wa Sekta ndogo za Uzalishaji Viwandani, Ujenzi na Umeme na Gesi.

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya Nje kwa mwaka 2014, mwenendo wa biashara na nchi za nje umezidi kuimarika kutokana na kuongezeka kwa thamani

ya usafirishaji wa bidhaa na huduma. Thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi iliongezeka kutoka TZS 87.6 bilioni mwaka 2013 kufikia thamani ya TZS 133.6 bilioni mwaka 2014. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa mazao ya biashara ya karafuu na mwani kutoka TZS 75.4 bilioni mwaka 2013 hadi 104.0 bilioni mwaka 2014.

Kwa upande wa thamani ya uagiziaji wa bidhaa kutoka nje, kumekuwa na ongezeko la asilimia 34.4 kutoka TZS 208.1 bilioni mwaka 2013 hadi kufikia thamani ya TZS 279.6 bilioni mwaka 2014, ambapo uagiziaji mkubwa ulionekana katika vyombo vya usafiri na mashine. Hali hii imepelekea kupanuka kwa urari wetu wa biashara za nje kwa kuongezeka nakisi kutoka TZS 120.5 bilioni mwaka 2013 hadi TZS 146.0 bilioni mwaka 2014.

Mhe. Spika, kwa upande wa utulivu wa bei, mwaka wa 2014 tumeendelea kuwa na mfumko wa bei ulio katika tarakimu moja. Hata hivyo, kiwango chake kimepanda kidogo kutoka wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2013 hadi asilimia 5.6 kwa mwaka 2014, kama ilivyoelezwa kwa undani zaidi katika Mapitio ya hali ya Uchumi leo asubuhi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitano (2010 hadi 2014), Pato la Taifa kwa bei za miaka husika limekua kutoka TZS 1,050.8 bilioni hadi kufikia TZS 2,133.5 bilioni. Kwa bei za kudumu, Pato la Taifa limekua kutoka TZS 848.2 bilioni hadi kufikia TZS 1,115.4 bilioni sawa na ukuaji wa asilimia 31.5 kwa kipindi hicho sawa na wastani wa ukuaji wa asilimia 6.3 kwa mwaka. Pato la Taifa kwa bei za miaka husika kwa mtu mmoja limekua kutoka TZS 856,000 ($613) mwaka 2010 hadi kufikia TZS 1,552,000 ($939) kwa mwaka 2014.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/11 hadi 2014/15, mapato ya ndani yameongezeka kutoka TZS 181.4 bilioni hadi kufikia TZS 360.4 bilioni 2014/15, sawa na ukuaji wa asilimia 98.7 kwa kipindi hicho au wastani wa asilimia 19.7 kwa kila mwaka.

## C. UTEKELEZAJI WA BAJETI

Mhe. Spika, itakumbukwa kuwa Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2014/15 ilipanga kukusanya TZS 707.8 bilioni. Kati ya fedha hizo TZS 386.8 bilioni ni kutoka vianzio vya ndani, ambapo *ZRB* ilitarajiwa kukusanya TZS 181.5 bilioni na *TRA* ilitarajiwa kukusanya TZS 166.0 bilioni. Mapato yaliyotarajiwa kukusanywa kutokana na vianzio visivyokuwa vya kodi (mapato ya mawizara) ni TZS 18.4 bilioni na kodi ya mapato ya wafanyakazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaofanya kazi Zanzibar (*PAYE*) ni TZS 21 bilioni.

Aidha, mapato yaliyotarajiwa kutoka nje ni TZS 306.0 bilioni zikiwemo TZS 40.0 bilioni kutokana na Misaada ya Kibajeti (*GBS*), TZS 66.3 bilioni kama ruzuku na TZS 199.1 bilioni ni mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo fedha kutokana na misamaha ya madeni ni TZS 0.6 bilioni. Serikali ilipanga kuchukua mikopo ya ndani ya muda mrefu ili kuziba nakisi ya TZS 15 bilioni.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi, Serikali ilipanga kutumia kiasi hicho cha TZS 707.8 bilioni, ambapo kazi za kawaida zilipangiwa kutumia TZS 376.5 bilioni wakati kazi za maendeleo zilitengewa TZS 331.3 bilioni. Kati ya fedha hizo za maendeleo, TZS 65.9 bilioni ni mchango wa Serikali na zilizosalia ni kutoka kwa mashirika ya Kimataifa na Washirika wa Maendeleo.

**Ukusanyaji halisi wa mapato ya ndani**

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2015, Serikali ilitarajia kukusanya jumla ya TZS 298.7 bilioni. Hata hivyo, jumla ya TZS 275.0 bilioni zimeweza kukusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 92.1 ya lengo la kipindi cha miezi tisa. Pamoja na kutofikiwa lengo la ukusanyaji wa mapato, kiwango hicho cha utendaji kinamaanisha ongezeko la mapato ya TZS 27.7 bilioni sawa na asilimia 10 ikilinganishwa na TZS 247.3 bilioni zilizokusanywa kipindi kama hiki cha miezi tisa mwaka 2013/14.

**Mapato ya Kodi**

Mhe. Spika, kwa kipindi cha miezi tisa hadi kufikia Machi 2015, mapato ya kodi yamefikia TZS 242.5 bilioni sawa na asilimia 91 ya lengo la TZS 266.4 bilioni. Kati ya mapato yaliyokusanywa, *ZRB* imeweza kukusanya jumla ya mapato ya kodi ya TZS 135.7 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 95 ya makadirio ya miezi tisa na *TRA* imekusanya jumla ya TZS 106.8 bilioni sawa na asilimia 86 ya makadirio ya miezi tisa.

**Mapato yasiyo ya Kodi**

Mhe. Spika, kwa upande wa makusanyo ya mapato yasiyokuwa ya kodi, jumla ya TZS 16.7 bilioni zimekusanywa sawa na asilimia 91 ya makadirio ya mwaka. Makusanyo hayo yanajumuisha mapato ya mawizara ya TZS 12.8 bilioni pamoja na gawio la faida kutoka Benki Kuu ya Tanzania TZS 3.2 bilioni na Mashirika ya Serikali ya TZS 0.7 bilioni.

**Mikopo ya Ndani**

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, Serikali imekopa ndani jumla ya TZS 10.1 bilioni sawa na asilimia 67 ya makadirio ya mwaka 2014/15 ukilinganisha na TZS 20.0 bilioni zilizokopwa katika kipindi kama hicho mwaka 2013/14.

**Matarajio ya mapato hadi Juni 2015**

Mhe. Spika, matarajio ya makusanyo hadi kufikia Juni 2015 ni TZS 375.4 bilioni sawa na asilimia 93 ya makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Kati ya Mapato hayo, TZS 360.1 bilioni ni mapato ya kodi na yasiyo ya kodi na TZS 15.0 bilioni ni mikopo ya ndani. Inatarajiwa kwamba *ZRB* itakusanya TZS 179.2 bilioni, *TRA* jumla ya TZS 140.7 bilioni, mapato yasiyokuwa ya kodi TZS 19.5 bilioni, *PAYE* kutoka SMT ni TZS 21.0 bilioni.

**Matumizi halisi**

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa hadi Machi 2015, Serikali imetumia jumla ya TZS 369.7 bilioni, ikiwa ni sawa na asilimia 52 ya malengo ya mwaka. Kati ya matumizi hayo, jumla ya TZS 261.2 bilioni zimetumika kwa ajili ya kazi za kawaida, sawa na asilimia 96 ya matarajio ya TZS 271.5 bilioni kwa kipindi hicho. Uchambuzi wa matumizi hayo ni kama hivi ifuatavyo:

a) Mishahara ni TZS 136.0 bilioni, sawa na asilimia 74 ya makadirio ya mwaka.
b) Matumizi mengineo ni TZS 44.0 bilioni, sawa na asilimia 61 ya makadirio ya mwaka.
c) Mfuko Mkuu wa Serikali ni TZS 48.4 bilioni, sawa na asilimia 69.3 ya makadirio ya mwaka, na
d) Ruzuku ni TZS 32.8 bilioni sawa na asilimia 65 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi katika shughuli za maendeleo, katika kipindi cha miezi tisa, Serikali imetumia jumla ya TZS 108.5 bilioni kwa ajili ya kazi za maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 32.7 ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo, Washirika wa Maendeleo wametoa TZS 69.4 bilioni sawa na asilimia 26 ya makadirio ya mwaka, (TZS 48.9 bilioni ni Ruzuku na TZS 20.5 bilioni ni Mikopo).

Mchango wa Serikali kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ulifikia TZS 39.1 bilioni sawa na asilimia 59 ya lengo la mwaka. Upatikanaji mdogo wa fedha za Washirika

wa Maendeleo umetokana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa baadhi ya miradi kama vile ujenzi wa jengo jipya la abiria katika uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume, ujenzi wa barabara za kati, Unguja na Mradi wa Huduma za Mijini (*ZUSP*).

**Deni la Taifa**

Mhe. Spika, deni la Taifa mpaka kufikia mwezi wa Machi 2015 limeongezeka hadi kufikia TZS 317.2 bilioni, sawa na ukuaji wa asilimia 7.6 ukilinganisha na deni lililokuwepo mwezi wa Machi 2014 la TZS 294.9 bilioni. Deni la Nje limefikia TZS 218 bilioni mpaka kufikia mwezi wa Machi 2015 ikilinganishwa na TZS 211.8 bilioni kufikia mwezi wa Machi 2014. Kati ya jumla ya madeni ya nje, asilimia 88 ilidhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na asilimia12 ilidhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Deni la ndani hadi mwezi wa Machi 2015 liliongezeka hadi kufikia TZS 99.3 bilioni ikilinganishwa na mwezi wa Machi 2014 la TZS 83.1 bilioni. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa deni la kiinua mgongo, deni la *ZSSF* na Hati Fungani kutoka Benki Kuu ya Tanzania yaani (*BOT*).

## D. UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO 2014/15

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15, serikali ilichukua hatua mbalimbali za kuimarisha mapato yake. Utekelezaji wa hatua hizo ni kama ifuatavyo:

**Kuimarisha usimamizi wa kimaeneo (*Block Management System*)**

(i) *ZRB* kwa kushirikiana na *TRA* na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa serikali imefanya mgawanyo wa maeneo kwa kutumia Teknohama (*GPS*) ili kupata taarifa zawafanyabiashara na maeneo walipo. Mpaka kufikia Machi 2015 Jumla ya wafanyabiashara wapya 830 tayari wamesajiliwa kulipa kodi kupitia utaratibu huu.

(ii) Kuzitambua na kuzichukulia hatua nyumba zote zinazotumiwa kulaza wageni ambazo hazijasajiliwa kulipa kodi. Katika zoezi la kuimarisha usimamizi wa kimaeneo, nyumba 12 katika maeneo ya ukanda wa mashariki na Nungwi zimetambuliwa na hatimae kusajiliwa kwenye mtandao wa kulipa kodi.

(iii) Kuanzishwa kwa utaratibu wa zuio katika ushuru wa stemp kutokana namafanikio yaliyopatikana katika *VAT*. Tayari Kanuni zimekamilishwa na kusainiwa na Waziri wa Fedha. Hatua za kuzitangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali zinaendelea.

(iv) Kuimarisha ukaguzi na upelelezi kwa walipakodi katika maeneo ya mawasiliano, utalii na nishati ya mafuta: Watendaji 3 wa *ZRB* wamepatiwa mafunzo na *TRA* (Tanzania Bara) juu ya upelelezi wa walipakodi, na watendaji 23 wamepatiwa mafunzo ya msingi ya ukaguzi katika sekta ya Utalii kupitia msaada wa Wizara ya Fedha ya Marekani (*US Treasury*) na Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*).

(v) Katika Kuimarisha matumizi ya Teknohama na usimamizi (supervision) kati ya *ZRB* na *TRA*. Kwa upande wa *ZRB*, Mtandao wa "*Zanzibar Integrated Tax Administration System*" (*ZITAS*) umeimarishwa na tayari unatoa huduma za kielektroniki kama ulivyokusudiwa. Idara ya Forodha imeendelea na matayarisho ya kutumia mfumo wa *Tanzania Customs Information System* (*TANCIS*) badala ya *ASYCUDA* na Idara ya Kodi za Ndani ya *TRA* nayo inatumia mfumo wa *Integrated Tax* (*ITAX*). Kwa sasa *TRA* na *ZRB* zinaendelea na mchakato wa kupitia mifumo yao na kuihakiki ili kuweza kuifanya iweze kuwasiliana (*interface*).

**1. Kuimarisha Uthamini wa Forodha**

Mhe. Spika, Eneo jengine lililoangaliwa na serikali kwa hatua za kiutawala ni uimarishaji wa uthamini wa bidhaa zinazoingizwa nchini (*Valuation*) kutokana na kuwepo kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu ambao hufanya udanganyifu, ukiwemo kushusha kiwango na thamani halisi ya bidhaa husika. Idara ya Forodha *TRA* inaendelea kukabiliana na tatizo hili ambapo imeanzisha *database* maalum kwa bidhaa zinazoingizwa mara kwa mara hapa Zanzibar. Kwa sasa, utiaji thamani wa bidhaa unazingatia thamani zilizomo katika *database* hiyo.

**Mapato yasiyokuwa ya kodi**

**2. Gawio kutoka kwa Mashirika ya Serikali**

Mhe. Spika, Serikali iliongeza kiwango cha gawio kutoka asilimia 10 hadi 20 kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015 kwa mashirika yanayomilikiwa na Serikali. Hadi kufikia mwisho wa Machi 2015, jumla ya TZS 727 milioni zimekusanywa kama gawio la faida iliyopatikana na mashirika hayo.

**3. Kupunguza kiwango cha ushuru wa Mirathi**

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/15, Serikali ilipunguza kiwango cha ushuru wa mirathi kutoka asilimia 5 hadi asilimia 0.25, Lengo ni kusajili mali na kupatikana kwa nyaraka halali za umiliki, ambazo zitawezesha kutumika katika shughuli mbali mbali za kiuchumi na kupunguza matatizo ya kijamii katika mirathi. Hatua zimechukuliwa pamoja na kufanyiwa marekebisho Kanuni ya

Ushuru wa Mirathi (*Estate Duty*), ambapo utekelezaji wake umeanza rasmi mwezi Februari 2015. Hadi kufikia Machi 2015, jumla ya TZS 4.2 milioni zimekusanywa.

**Marekebisho ya Sheria za kodi**

**4. Sheria ya Usimamizi wa kodi namba 7 ya mwaka 2009.**

Mhe. Spika, Serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ya Usimamizi wa kodi *TAPA* kwa kubadilisha tarehe ya kuwasilisha ritani na kufanya malipo, ambapo awali tarehe ya kuwasilisha ritani ni tarehe 15 na kufanya malipo tarehe 25. Marekebisho ya sasa ni kuwasilisha ritani tarehe 7 na malipo ni tarehe 15. Marekebisho haya yamesaidia kuiwezesha serikali kupata mapato yake mapema zaidi na kuweza kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

**5. Sheria ya Ada za Bandari namba 2 ya mwaka 1999.**

Mhe. Spika, Baraza liliidhinisha pia marekebisho ya Sheria ya Ada ya Bandari kwa kuongeza Ada ya Usalama wa Uwanja wa Ndege kwa abiria anaesafiri ndani ya Tanzania kutoka kiwango cha malipo kwa abiria wa ndani cha TZS 1,000 hadi TZS 3,000. Jumla ya TZS 2.07 bilioni zimekusanywa hadi kufikia Machi 2015.

**6. Sheria ya Usafiri wa Barabara Namba 7 ya mwaka 2003.**

Mhe. Spika, Baraza lako liliridhia kubadilisha muda wa utoaji wa leseni za udereva na malipo ya leseni hizo. Chini ya marekebisho hayo, tayari leseni zinatolewa kwa muda wa miaka miwili, mitatu na mitano na viwango vya malipo kwa leseni ni TZS 35,000, TZS 45,000 na TZS 60,000 kwa lengo la kupunguza usumbufu kwa madereva kulazimika kurudi kila mwaka kuhuisha leseni. Jumla ya TZS 979.1 milioni zimekusanywa katika kipindi cha miezi tisa sawa na ongezeko la asilimia 59.7 au TZS 366 milioni.

**7. Kupunguza Misamaha ya kodi.**

Mhe. Spika, Baraza pia lilikubali pendekezo la Serikali la kupunguza misamaha ya kodi kwa wawekezaji kutoka asilimia 80 hadi asilimia 75 kwa uingizaji wa vifaa vya uwekezaji nchini. Kutokana na mabadiliko hayo, tokea mwezi Julai 2014 wawekezaji hulipa asilimia 25 ya kodi yote ya vifaa vilivyosamehewa kodi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kuhusu utekelezaji wa hatua za kuimarisha mapato kwa mwaka 2014/15, naomba sasa nitoe mwelekeo wa Bajeti ya mwaka 2015/16.

## E. MWELEKEO WA BAJETI 2015/16

### Malengo Makuu ya Serikali

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa Fedha wa 2015/16, Bajeti itaendelea kuzingatia malengo makuu ya Serikali. Malengo hayo ni Kujenga jamii:

(i) Iliyo elimika kwa Elimu bora na inayotoa wataalamu wenye hadhi ya kimataifa;
(ii) Yenye siha;
(iii) Iliyoimarika kiuchumi; na
(iv) Inayojali umoja wa kitaifa na kufuata misingi ya utawala bora.

Mambo haya ndio yanayojenga falsafa iliyomo katika Dira ya Maendeleo ya 2020 ambayo inatekelezwa kwa sasa kupitia MKUZA II na Mpango wake wa utekelezaji. Utendaji wa Sekta zote umejielekeza katika kufikiwa kwa malengo hayo makuu.

## F. MAKADIRIO YA MAPATO KWA 2015/2016

Mhe. Spika, Serikali imekadiria kukusanya jumla ya TZS 830.4 bilioni ambapo mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia TZS 450.5 bilioni na mapato ya nje kwa miradi ya maendeleo ni TZS 347.1 bilioni. Aidha, fedha kutokana na msamaha wa madeni yanatarajiwa kufikia TZS 1.3 bilioni na Mfuko wa Wafadhili ni TZS 1.5 bilioni. Mikopo ya ndani inatarajiwa kufikia TZS 30.0 bilioni.

### Makadirio ya Mapato ya Ndani

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/16, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya mapato ya ndani ya TZS 450.5 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 25 ya matarajio ya mapato ya mwaka 2014/15 ya TZS 360.4 bilioni.

### Mapato ya Kodi

Mhe. Spika, jumla ya TZS 404.5 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kutokana na mapato ya kodi mbalimbali. Mapato haya yanahusisha hatua mpya za mapato zinazopendekezwa kutekelezwa kwa mwaka ujao wa fedha ambazo nitaziwasilisha baadae. Kati ya kiasi hicho cha mapato, *TRA* inatarajiwa kukusanya TZS 178.6 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 27 ya kiasi kinachotarajiwa kukusanywa hadi Juni 2015 wakati *ZRB* inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 225.9 bilioni, sawa na ongezeko la asilimia 26 ya matarajio  ya makusanyo ya mwaka 2014/15.

**Kodi ya PAYE kutoka Tanzania Bara**

Mhe. Spika, Jumla ya TZS 21.0 bilioni zinakadiriwa kukusanywa kutokana na mishahara ya wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaofanya kazi Zanzibar.

**Mapato yasio ya Kodi**

Mhe. Spika, mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 25 bilioni, yakimaanisha ongezeko la asilimia 28 kutoka jumla ya TZS 19.5 bilioni zinazotarajiwa kukusanywa hadi Juni 2015.

**Mikopo ya Ndani**

Mhe. Spika, kama nitakavyobainisha baadae, Serikali inategemea kukopa ndani TZS 30 bilioni kwa ajili ya kufidia nakisi iliyojitokeza katika bajeti ya mwaka 2015/16.

**Mapato ya Nje (Ruzuku na Mikopo)**

**Misada ya Kibajeti**

Mhe. Spika, serikali imekuwa ikipokea Misaada ya Kibajeti (*General Budget Support - GBS*) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Misaada hii imekuwa chachu muhimu katika utekelezaji wa Bajeti yetu hususan katika kuimarisha uwezo wa serikali kwenye Miradi ya Maendeleo. Kwa bahati mbaya, kwa miaka kadhaa sasa kumekuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa *GBS* kutokana na sababu mbalimbali, miongoni mwake ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:

i. Matatizo ya kifedha katika nchi za Washirika wenyewe;
ii. Mwenendo wa kiuchumi ikiwemo mgogoro wa kifedha duniani;
iii. Masuala ya utawala bora nchini hasa tuhuma za rushwa na matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mhe. Spika, kadhia ya hivi karibuni iliyopelekea Washirika wa Maendeleo kuzuia misaada ya *GBS* ni kashfa ya matumizi ya fedha katika Hesabu ya Escrow ya Tegeta huko Tanzania Bara. Wafadhili wamezuia tena misaada ya *GBS* ili kuishinikiza Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuchukua hatua juu ya watu waliotuhumiwa kuhusika pamoja na hatua nyengine za kuimarisha mfumo wa usimamizi. Pamoja na kwamba kashfa zinazotokea Tanzania Bara hazikuihusu Zanzibar kwa namna yoyote ile, bado kuzuiwa kwa *GBS* kumekuwa na athari kubwa kwa utekelezaji wa Bajeti ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ili kuepusha athari kubwa kwa utekelezaji wa Bajeti, kuanzia mwaka wa fedha wa 2015/16, imeamuliwa kutoingiza moja kwa moja makadirio ya *GBS* katika Bajeti ya Serikali. Badala yake, utaratibu maalum umewekwa wa kuwezesha kupokea na kutumia fedha hizo pindi zikipatikana.

**Mikopo na Ruzuku kwa Miradi ya Maendeleo**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya TZS 347.1 bilioni zinatarajiwa kupokelewa kutoka kwa Taasisi za Kimataifa na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kutekeleza Programu na Miradi ya Maendeleo. Kiasi hicho kinaashiria kuongezeka kwa misaada kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo kwa asilimia 48 kutoka TZS 127.9 bilioni zinazotarajiwa kupatikana hadi Juni 2015. Sababu kubwa ya ongezeko ni ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa ndege wa Abeid Aman Karume ambao unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka ujao wa fedha. Sehemu kubwa ya fedha zilizobakia kwa ujenzi huo zinatarajiwa kulipwa katika kipindi hicho. Kati ya fedha zinazotarajiwa kwa mwaka 2015/16, Ruzuku ni TZS 98.2 bilioni na Mikopo ni TZS 248.9 bilioni.

## G. HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO 2015/16

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema, Serikali inakusudia kuchukua hatua kadhaa ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani. Haja hii imetokana sio tu na mwenendo usioridhisha wa Misaada ya Kibajeti (*GBS*) kama nilivyoelezea awali, lakini pia dhamira ya Serikali ya kuharakisha maendeleo huku ikizidisha kasi ya kupunguza utegemezi wa misaada. Kama ilivyo kawaida, ili kufikia lengo hilo, kuna hatua za kiutawala na zile za kubadilisha Sheria zinapaswa kutekelezwa.

**Hatua za Kiutawala**

Mhe. Spika, Kwa upande wa hatua za kiutawala, maeneo yatakayosimamiwa kwa karibu ni pamoja na haya yafuatayo:

**1. Upimaji wa Ardhi**

Mhe. Spika, Moja ya misingi muhimu ya mfumo wa kodi ni kuwepo kwa usawa miongoni mwa walipakodi. Imegundulika kuwa maeneo mengi ya kibiashara katika Mkoa wa Mjini Magharibi hayajapimwa na hayalipiwi kodi ya ardhi. Hali hii inakwenda kinyume na matakwa ya mfumo bora wa kodi. Kwa mwaka wa fedha ujao, Serikali kupitia Idara ya Ardhi kwa kushirikiana na taasisi za kodi, itaanza kuyapima maeneo ya kibiashara ambayo hayajapimwa ili kuhami mapato yake na kuwa na mfumo wa haki kwa walipakodi wote. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali ya jumla TZS 262 milioni.

**2. Bodi ya Kusimamia Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu.**

Mhe. Spika, maeneo mengine ya kiutawala ni kutekeleza uanzishaji wa Bodi ya Kusimamia Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu nchini na kuanzisha matumizi ya mashine maalum za kutolea risiti kwa njia ya elektroniki (*Electronic Fiscal Devices* - *EFDs*). Matayarisho ya mambo haya tayari yamefikia hatua ya kuridhisha na yanatarajiwa kuanza rasmi katika mwaka wa fedha 2015/16. Jumla ya TZS 6.0 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kutokana na hatua hizo.

**Mapato Yasiyokuwa ya Kodi**

**3. Kufanya Mapitio ya Viwango vya Ada mbali mabli zinazotozwa na Taasisi za Serikali**

Mhe. Spika, Imebainika kwamba mapato yanayokusanywa na taasisi mbalimbali za Serikali bado yako chini sana, hali hii imekuwa ikisababishwa na viwango vya ada hizo kuwa vya zamani na kutoendana na wakati. Serikali inakusudia kuvifanyia mapitio viwango vya ada katika taasisi za Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali; Wizara ya Afya; Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko; na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Idara Maalum ili viendane na wakati bila ya kuathiri utoaji wa huduma hizo. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya jumla ya TZS 60 milioni.

**Marekebisho ya Sheria za Kodi**

**4. Kodi ya Miundombinu (*Infrastructure Tax*)**

Mhe. Spika, Kwa sehemu kubwa uimarishaji wa miundombinu nchini umekuwa ukitegemea mchango wa ruzuku kutoka Taasisi za fedha za kimataifa na Washirika wa Maendeleo. Wakati bado kuna uhaba wa miundombinu muhimu, mwenendo wa Washirika wa Maendeleo umekuwa hautabiriki na una muelekeo wa kupungua mwaka hadi mwaka. Serikali inalazimika kubuni utaratibu maalum ili iweze kuwekeza zaidi katika eneo hili muhimu. Kuanzia mwaka ujao wa Fedha, inapendekezwa kuanzisha Kodi maalum kwa ajili ya miundombinu (*Infrastructure Tax*). Mapato yatakayopatikana kutokana na Kodi hizo yatawekwa katika Mfuko maalum (*Infrastructure Fund*). Mapato hayo yatatokana na mabadiliko ya kodi mbalimbali ambapo kwa mwaka wa fedha 2015/16, jumla ya TZS 25 bilioni zinatarajiwa kukusanywa. Asilimia 75 ya fedha zitakazopatikana zitaelekezwa katika uimarishaji wa miundombinu muhimu na asilimia 25 iliyobakia itatumika kwa ajili ya Mifuko mingine iliyoanzishwa chini ya Sheria mbali mbali. Mgao wa fedha hizo za asilimia 25 kwa ajili ya Mifuko hiyo utaandaliwa utaratibu maalum.

Mhe. Spika, kati ya TZS 25 bilioni, TZS 10 bilioni zinatarajiwa kukusanywa na *TRA* kupitia Idara ya Forodha na TZS 15 bilioni zitakusanywa na *ZRB* kama kodi za ndani. Kodi hiyo itatozwa chini ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2015 na usimamizi wake utafuata Sheria ya Usimamizi wa Kodi (*TAPA*) namba 7 ya mwaka 2009. Kodi zinazopendekezwa kutozwa kwa madhumuni ya

Miundombinu ni kama ifuatavyo:

i. Kutoza Dola moja ya Kimarekani kwa siku kwa kila mgeni atakaelala katika hoteli za Zanzibar ambapo itachangia TZS 3.2 bilioni;

ii. Kutoza TZS 2,000 kwa kila abiria anaeondoka katika Bandari za Zanzibar kwenda katika Bandari nyengine za Tanzania nje ya Zanzibar na TZS 2,000 kwa kila abiria anaeondoka katika Bandari za Zanzibar kwenda katika Bandari nyengine za Zanzibar. Jumla ya TZS 1.9 bilioni zinatarajiwa kupatikana kutokana na hatua hii;

iii. Kutoza TZS 2,000 kwa kila abiria anaeondoka katika Kiwanja cha Ndege kilichopo Zanzibar na kwenda kiwanja chengine ndani ya Tanzania. Jumla ya TZS 684 milioni zinatarajiwa kukusanywa;

iv. Kutoza asilimia 3 ya thamani za bidhaa zinazoingizwa nchini ambapo jumla ya TZS 10.0 bilioni zinatarajiwa kukusanywa;

v. Kutoza asilimia 2 kwa ununuzi wa umeme na kutarajiwa kuingiza TZS 0.9 bilioni; na

vi. Kutoza TZS 100/= ya ziada kwa lita ya Petroli au Dizeli inayoingizwa nchini. Hatua hii inatarajiwa kuingiza jumla ya TZS 8.3 bilioni. Kwa ujumla, hatua zote hizo zinatarajiwa kuingiza jumla ya TZS 25.0 bilioni.

**5. Ada ya Viwanja vya Ndege na Bandari (Sheria ya Ada ya Bandari Namba 2 ya Mwaka 1999)**

Mhe. Spika, Kampuni za Ndege zinazotoa huduma za usafiri hapa Zanzibar, huwatangazia abiria wanaosafiri kwenda nje ya Tanzania Dola 9 kwa mujibu wa Sheria ya Tanzania Bara kwa kila abiria kama ni ada ya usalama wa uwanja wa ndege. Kampuni hizo hukusanya ada hiyo na huwasilisha malipo ya Dola 8 kwa

kila abiria kwa mujibu wa Sheria ya Zanzibar. Ili kurekebisha kasoro hiyo inapendekezwa kuongezwa ada hiyo kutoka Dola 8 hadi 9 ili kutambua rasmi ada hiyo inayotozwa sasa.

Mhe. Spika, Kwa upande wa Bandari, Serikali inajukumu la kuimarisha huduma katika Bandari zake,Unguja na Pemba. Hivyo, inapendekeza kuongeza tozo la mauzo ya tiketi na usafirishaji wa mizigo baharini kutoka asilimia 5 ya sasa hadi asilimia 8.

Hatua hizi zinatarajiwa kuingizia Serikali jumla ya TZS 969 milioni.

**Kuondoa misamaha ya kodi ya mapato *(Tax Holidays)* na kuruhusu punguzo la Uchakavu kwa haraka Zaidi *(Accelerated Depreciation)***

Mhe. Spika, Mfumo uliopo sasa wa kutoa misamaha kwa wawekezaji wa ndani na nje katika kodi ya mapato itokanayo na faida *(Corporate Income Tax Holiday*) umepitwa na wakati, na hauendani na mahitaji ya uwekezaji. Miongoni mwa changamoto zinazokabili mfumo huu ni kama zifuatzo:-

1. Kutokuwepo kwa usawa katika utowaji wa misamaha kwa miradi ya wawekezaji ambapo miradi yenye kurejesha gharama kwa haraka *(higher rate of return)* inapatiwa msamaha sawa na ile inayorejesha taratibu *(lower rate of return);*

2. Kuwezesha uhamishaji wa faida kutoka kampuni moja kwenda nyengine zinazomilikiwa na mtu mmoja *(domestic transfer pricing);*

3. Unawezesha mwekezaji kupatiwa msamaha wa kodi na baada ya kumalizika kwa muda wa msamaha huo anafunga biashara/anauza mradi na hatimae kuja mwekezaji mwengine na kudai tena msamaha;

4. Unavutia zaidi miradi midogo midogo kuliko miradi mikubwa; na

5. Unapelekea kutokujulikana kiwango sahihi cha misamaha ya kodi inayotolewa na Serikali.

Mhe. Spika, Ili kuondokana na changamoto hizo inapendekezwa kubadilisha mfumo wa sasa na kwenda na mfumo wa *"Accelerated Depreciation"* ambao unaruhusu msamaha kwa vifaa vilivyowekezwa na kutumika katika mradi. Marekebisho haya yatafanywa chini ya Sheria ya kulinda Vitega Uchumi namba 11 ya mwaka 2004.

Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato jumla ya TZS 500 milioni kwa mwaka 2015/16. Mafanikio zaidi ya ukusanyaji yanatarajiwa miaka inayofuata baada ya kumaliza kipindi cha msamaha kwa wawekezaji wenye msamaha huo kwa sasa hivi.

**Sheria ya Usajili wa Kampuni**

Mhe. Spika, kutokana na gharama kubwa za kusajili jina la biashara zinazowakabili wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, wawekezaji hao hupunguza kiwango cha mtaji wanaposajili jina la biashara. Kuanzia mwaka wa fedha wa 2015/16 inapendekezwa kupunguza gharama za kusajili jina la biashara na kuwa TZS 5,000 tu kutoka asilimia moja ya mtaji.

**Kupunguza Misamaha ya Kodi (Sheria ya kodi ya Ongezeko la Thamani Namba 4 ya mwaka 1998)**

Mhe. Spika, Ili kuimarisha mapato ya Serikali, katika mwaka unaoendelea wa fedha, Serikali ilipunguza unafuu wa misamaha ya Ushuru na Kodi ya *VAT* kwa wawekezaji. Hatua hii haikuhusisha Taasisi za kijamii (*NGOs*) na za kidini. Kwa mwaka wa fedha 2015/16 inapendekezwa kupunguza kiwango cha unafuu maalum kwa kodi ya *VAT* kwa taasisi za kijamii na kidini hadi kufikia asilimia 75 kama inavyoonekana katika vifungu vya (k), (i) na (m) vya jadweli ya 3 ya Sheria ya *VAT*. Kwa mabadiliko haya, Taasisi hizo sasa zitapaswa kulipa asilimia 25 ya Kodi na kusamehewa asilimia 75 iliyobakia kwa vifaa vinavyostahiki msamaha. Lengo la hatua hii ni kuwianisha viwango vya misamaha baina ya ile inayotolewa kwa wawekezaji ambao tayari unafuu wao ni asilimia 75 na misamaha inayotolewa kwa Taasisi zisizo za Kiserikali.

Hata hivyo, Serikali itaendelea kutoa msamaha wa asilimia 100 kwa taasisi hizo za kijamii na kidini kwa ajili ya shughuli za misaada wakati wa maafa na pia katika miradi inayotekelezwa pamoja na Serikali katika huduma za maji, afya na elimu. Hatua hii haitarajiwi kuongeza sana mapato, bali inakusudia kuleta uwiano wa misamaha baina ya wawekezaji na taasisi zisizo za kiserikali na hivyo kurahisha usimamizi wa Kodi.

**Ada ya Uingizaji wa Magari.**

Mhe. Spika, Serikali, kupitia Shirika la Magari, ilikuwa ikitoza Ada ya TZS 100,000 kwa magari yote yanapoingia nchini. Kufuatia kufungwa rasmi Shirika hilo, kwa sasa mapato haya yanakusanywa na *TRA* na kuingizwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa mwaka wa fedha ujao, inapendekezwa kubadilisha kiwango hicho na

kuweka kiwango mbadala cha ama TZS 100,000 kwa gari au aslimia 3 ya thamani ya gari inayoingizwa kwa kufuata kiwango kinachotoa mapato zaidi. Marekebisho haya yatafanywa kupitia Kanuni zilizo chini ya Sheria ya Biashara, namba 14 ya mwaka 2013. Hatua hii itaongeza mapato ya Serikali kwa jumla ya TZS 800 milioni.

Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa gharama za matengenezo ya barabara kutokana na kupanuka kwa mtandao wa barabara nchini, mapato yatakayopatikana kutokana na ada hii yatapelekwa Mfuko wa Barabara ili kusaidia zaidi matengenezo ya barabara.

**Msamaha wa Ushuru wa Forodha kwa Majiko (Stoves) yanayotumia *Ethanol* iliyosarifiwa**

Mhe. Spika, Ripoti za tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa bado wananchi wengi wanatumia kuni na bidhaa za kuni kama vile makaa kwa ajili ya nishati ya kupikia nyumbani. Hali hii inaendelea kuathiri mazingira yetu na vyanzo vya maji kutokana na ukataji mkubwa wa misitu ya asili. Katika miaka ya karibuni baadhi ya wananchi wameanza kutumia gesi ya asili katika matumizi ya nyumbani. Hata hivyo, bado matumzi hayo hayajakuwa kwa kiasi cha kutosha kupunguza matumizi ya kuni na makaa. Kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda, *UNIDO*, utafiti umefanywa juu ya matumizi ya majiko yanayotumia spiriti ya aina ya ethanol.

Mhe. Spika**,** matokeo ya utafiti huo yameonesha matumaini makubwa kwa upande wa unafuu wa gharama, nishati inayopatikana na ufanisi wake. Kwa kuwa jitihada za Serikali za kufufua kiwanda cha Sukari cha Mahonda kupitia uwekezaji binafsi zinaendelea, na inatarajiwa kuwa miongoni mwa bidhaa za ziada zitakazozalishwa kiwandani hapo ni ethanol, kuna haja ya kuanza kushajiisha matumizi ya majiko maalum yanayotumia aina hii ya nishati. Serikali inapendekeza kuondoa ushuru kwa majiko hayo. Aidha, hadi hapo spiriti ya ethanol itakapotengenezwa ya kutosha nchini, inapendekezwa pia kuondoa ushuru wa forodha kwa uingizaji wa ethanol iliyosarifiwa maalumu kwa matumizi ya nishati. Kwa kuwa kwa sasa majiko haya hayaingizwi, hatua hii haitarajiwi kuleta athari ya mapato.

Mhe. Spika, Serikali itahakikisha kuwa kuna usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa mapato kwa taasisi zote ili kuhakikisha malengo waliyowekewa yanafikiwa. Usimamizi huo utajumuisha kuzipitia mara kwa mara taasisi husika kwa kuzifanyia tathmini na kuzikagua ili kujua changamoto zilizopo kwa lengo la kuimarisha vyanzo vya ukusanyaji wa mapato. Aidha, Wakuu wa Taasisi wanatakiwa wawe makini katika kusimamia mapato ya taasisi zao ili kufanikisha shabaha zilizowekwa.

## H. MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA 2015/16

Mhe. Spika**,** kwa mwaka 2015/16 jumla ya TZS 830.4 bilioni zimekadiriwa kutumika kwa kazi za kawaida na maendeleo. Kwa upande wa matumizi ya kazi za kawaida, Serikali inatarajia kutumia jumla ya TZS 431.4 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 26 ikilinganishwa na TZS 343.4 bilioni zitakazotumika mwaka 2014/15. Kwa upande wa kazi za maendeleo, jumla ya TZS 399.0 bilioni zinatarajiwa kutumia ikiwa ni ongezeko la asilimia 122 kwa kulinganishwa na TZS 179.7 bilioni zinazotarajiwa kutumika hadi Juni 2015. Ongezeko hilo kubwa linatarajiwa kutokana na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo jipya la abiria katika kiwanja cha ndege cha Abeid Amani Karume. Fedha hizo, zinatarajiwa kuongeza pia mchango wa Washirika wa maendeleo kwa asilimia 171 kutoka TZS 127.9 bilioni zinazotarajiwa kutumika hadi Juni 2015 hadi kufikia TZS 347.1 bilioni kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Mhe. Spika**,** Serikali inatarajiwa kuchangia jumla ya TZS 51.9 bilioni kama mchango wake kwa kazi za Maendeleo sawa na matumizi ya TZS 51.8 bilioni ya mwaka 2014/15.

## MAENEO MUHIMU YALIYOZINGATIWA KATIKA BAJETI YA MWAKA 2015/16

Mhe.Spika, Serikali ni ya Wananchi na siku zote huwa inafanyakazi kwa ajili yao. Kwa kutambua ukweli huu, Bajeti ya Serikali itaendelea kuelekeza fedha katika maeneo makubwa yanayowagusa wananchi. Kwa mwaka ujao wa Fedha, maeneo muhimu yaliozingatiwa ni pamoja na haya yafuatayo:

### Miundombinu

Mhe. Spika**,** nchi yetu bado ni miongoni mwa nchi maskini zaidi duniani na ni nchi inayoendelea. Kwa kawaida, nchi zilizomo katika kundi hili huwa na uhaba wa miundombinu mbalimbali muhimu ikiwemo ya nishati, barabara, viwanja vya ndege, bandari, na maji. Kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali imetenga jumla ya TZS 212.4 bilioni kwa kazi za maendeleo katika Sekta za Miundombinu na Mawasiliano na Maji na Nishati pekee. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 53.2 ya Bajeti yote ya Kazi za Maendeleo.

**Huduma za Elimu**

Mhe. Spika, kulingana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012, Zanzibar kwa sasa inakisiwa kuwa na watu wapatao 1,375,000. Asilimia 42.5 ya idadi yote ni watoto walio na umri wa chini ya miaka 15. Aidha, asilimia 20.3 ya idadi yote ni watu walio na umri wa kati ya miaka 15 na 24. Takwimu pia zinaonesha kuwa kwa mwaka 2014, watoto wapatao 253,152 walikuwa katika skuli za msingi, kati yao 233,883 wakiwa katika skuli za Msingi za Serikali, sawa na asilimia 92.4 ya wanafunzi wote wa Skuli za Msingi. Aidha, takwimu pia zinaonesha kuwa kwa mwaka huo, tulikuwa na wanafunzi 81,621 katika Skuli za Sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita. Kati yao, wanafunzi 74,968 sawa na asilimia 91.8 walikuwa katika Skuli za Serikali. Kwa upande wa Elimu ya juu, takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka huo tulikuwa na zaidi ya wanafunzi 11,000 katika vyuo mbalimbali vilivyopo Zanzibar pekee.

Mhe. Spika, takwimu hizi zinamaanisha kwamba kwa ujumla, jamii yetu kwa kiasi kikubwa inaundwa na vijana, hasa watoto wa chini ya miaka 25 ambao kwa ujumla wanafikia asilimia 62.8 ya watu wote wa Zanzibar. Kundi hili lina mahitaji maalum. Kwa umri wa kuwa skuli, mahitaji muhimu zaidi ni elimu. Serikali inatambua wajibu wake wa kutoa Elimu iliyo bora kwa watoto wetu wote. Kwa sababu hii, jumla ya TZS 120.7 bilioni sawa na asilimia 14.5 ya Bajeti yote zimetengwa kwa ajili ya Sekta ya Elimu. Sekta hii pia ndio inayoongoza kwa Bajeti ya Kazi za kawaida kwa kutengewa TZS 96.8 bilioni, sawa na asilimia 22 ya Bajeti yote ya kazi za kawaida.

Mhe. Spika, kutokana na matumizi hayo, na kwa kuzingatia Sera ya Elimu Bila ya Malipo iliyotangazwa mara tu baada ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964, na kama ilivyoelezwa katika Mpango wa Maendeleo uliowasilishwa leo kuwa mojawapo ya vipaumbele ni kutoa elimu iliyo bora, Serikali inakusudia kuchukua hatua mahsusi zinazolenga kubeba zaidi jukumu la kutoa elimu kwa watoto wetu. Naomba nitamke rasmi kuwa kuanzia mwaka wa fedha 2015/16, michango yote wanayotozwa wazazi kwa elimu ya watoto wa skuli za msingi imefutwa. Hakuna mzazi atakaetozwa malipo yoyote kwa mtoto anaesoma skuli ya Msingi ya Serikali. Serikali itabeba jukumu la kuwasomesha watoto wote.

Mhe. Spika**,** Kwa upande wa Elimu ya Sekondari, Serikali inajipanga ili nako elimu yote iweze kutolewa bila ya malipo. Kwa kuanzia, kwa mwaka wa fedha 2015/16, Serikali inafuta rasmi malipo yote yanayotozwa wazee kwa ajili ya mitihani ya Kidato cha pili, kidato cha nne na kidato cha sita**.** Wazazi hawatatozwa tena malipo yoyote ya mitihani ya sekondari kwa watoto wao. Serikali inabeba pia jukumu hili.

Kwa kutekeleza azma hiyo ya Serikali ya kuwaondoshea wazee michango ya elimu ya Msingi na malipo kwa ajili ya mitihani ya Sekondari, Serikali imetenga jumla ya TZS 8.0 bilioni kwa mwaka ujao wa fedha 2015/16. Aidha, jumla ya TZS 9.5 bilioni zimetengwa kwa ajili ya Ruzuku kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Tokea kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu mwaka 2011, Serikali imeshatowa Zaidi ya TZS 26 bilioni kwa ajili ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

**Huduma za Afya**

Mhe. Spika, sekta nyengine muhimu na inayomgusa takriban kila mwananchi ni sekta ya Afya. Takwimu za Sensa ya Watu na Makaazi zinaonesha kuwa asilimia 15.6 ya wakaazi wote wa Zanzibar ni watoto wa chini ya umri wa miaka mitano. Kwa takwimu za sasa za idadi ya watu, watoto wa kundi hili wanafikia 214,500. Watoto hawa wana mahitaji maalum ya afya, hususan chanjo dhidi ya maradhi mbalimbali.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, Utafiti wa Kijamii na Uchumi wa mwaka 2015 unaonesha kuwa kwa mwaka 2014, jumla ya wagonjwa 440,201 walitibiwa katika hospitali za Serikali. Hali hii inaonesha kupungua kwa wagonjwa kutoka wagonjwa 456,750 waliotibiwa mwaka 2013. Kama nilivyotamka awali kuwa moja ya malengo makuu yaliomo katika falsafa ya Dira ya Maendeleo ni kujenga Taifa la watu wenye siha, uimarishaji wa Sekta ya afya una umuhimu wa pekee. Kwa kuzingatia dhima hii, Serikali imetenga jumla ya TZS 85.0 bilioni sawa na asilimia 10.2 ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2015/16 kwa Sekta ya Afya na hivyo kuifanya kuwa sekta ya tatu kifedha ikitanguliwa na Miundombinu na Elimu.

Mhe. Spika, miongoni mwa maeneo muhimu katika uimarishaji wa Afya ni upatikanaji wa Dawa, vifaa vya tiba na nyenzo nyengine muhimu. Kwa miaka kadhaa sasa sehemu kubwa ya dawa kwa ajili ya Hospitali zetu imekuwa ikipatikana kwa msaada wa Washirika wa Maendeleo hususan Shirika la Maendeleo la Denmark, *DANIDA*. Hata hivyo, Taarifa zilizopo sasa zinaashiria kuwa *DANIDA* imeanza kupunguza msaada wake kwa Sekta ya Afya. Pamoja na hali hiyo, kwa niaba ya Serikali na wananchi wote wa Zanzibar naomba nitumie fursa hii kulishukuru kwa dhati kabisa Shirika la *DANIDA* kwa msaada wake katika kipindi chote hicho, msaada ambao umenusuru maisha yetu na wananchi wenzetu. Serikali kwa kutambua dhima yake katika upatikanaji wa dawa, vifaa vya tiba na vifaa vyenginevyo, imefanya uamuzi wa kubeba jukumu hili kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa Bajeti ya mwaka 2015/16 jumla ya TZS 4.5 bilioni zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa mbalimbali vya tiba.

Mhe. Spika, Serikali imekuwa ikipeleka nje ya nchi, hususan nchini India, wagonjwa ambao matibabu yao yameshindikana hapa nchini. Pamoja na gharama

za matibabu nje ya nchi kuwa kubwa sana, bado utaratibu huu umesaidia sana ama kuokoa maisha ya wananchi wenzetu au kuwaondoshea maradhi yalioshindikana hapa nchini. Kwa bahati mbaya, fedha zilizokuwa zikitengwa kwa madhumuni haya ni kidogo wakati mahitaji yake ni makubwa sana. Kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali imetenga jumla ya TZS 2.5 bilioni kwa madhumuni hayo hii ni zaidi ya asilimia 213 ya iliotengwa kwa ajili ya mwaka 2015/16. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba utaratibu huu umewekwa kwa wenzetu ambao matibabu yao hayapatikani hapa nchini. Jitihada za kudhibiti matumizi ya fursa hii zitaimarishwa ili kuhakikisha unanufaisha wale tu wanaohitaji kweli matibabu nje ya nchi.

**Huduma kwa Wazee**

Mhe. Spika, kundi jengine muhimu kwa jamii yetu ni Wazee. Kundi hili pia lilipewa umuhimu maalum tokea Mapinduzi yetu matukufu kwa kupatiwa makaazi na matunzo maalum. Taarifa ya Sensa ya mwaka 2012 inaonesha kuwa Wazee waliofikia miaka 65 na zaidi ni asilimia 2.8 ya watu wote wa Zanzibar. Hawa ni wazee wetu ambao wameshatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu, ulezi wa vijana na watoto na sasa wamefikia umri wa kusaidiwa. Takwimu zinaonesha kuwa idadi ya wazee wanaohitaji msaada wa matunzo ya Serikali imekuwa ikipungua kutoka Wazee 223 mwaka 2010 hadi Wazee 148 mwaka 2015. Hali hii inamaanisha kuwa wengi wa Wazee wetu wanatunzwa na jamii, hasa watoto na jamaa zao. Baadhi ya Wazee hawa ni wale waliotumikia Serikali wakati wa ujana wao na kwa sasa ni Wastaafu na wanategemea kipato cha pencheni.

Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko ya udogo wa kiwango cha chini cha pencheni kinachotolewa na serikali. Serikali iliahidi kukiangalia kiwango hicho kwa kadiri hali inavyoturuhusu hasa kwa kuzingatia kuwa mara kadhaa kumekuwa na marekebisho ya mishahara kwa wafanyakazi wa serikali ambayo hayakuhusisha pencheni.

Kwa mwaka wa fedha 2015/16, Serikali inakusudia kupandisha kiwango cha chini cha pencheni kutoka TZS 40,000 kwa mwezi za sasa hadi TZS 60,000. Marekebisho haya yamelenga zaidi kwa wale ambao wanapokea kiwango cha chini cha pencheni.

Mhe. Spika, baadhi ya nchi duniani zina utaratibu wa kulipa pencheni kwa wazee hata kama sio wastaafu wa serikalini. Katika nchi za jirani kama vile Mauritius, utaratibu huu umetumika kwa miaka kadhaa sasa. Serikali kwa kusaidiana na Taasisi ya kuwasaidia wazee ya *"Help Age International"* imefanya utafiti na kuzingatia uzoefu wa nchi nyengine katika kutunza wazee. Kwa sasa serikali inakamilisha taratibu za kuwatambua Wazee wote waliofikia miaka 70 na zaidi

kwa lengo la kuwapatia vitambulisho vyao pamoja na taratibu nyengine. Zoezi hili litachukua sio zaidi ya miezi 10.

Nina furaha kulitangazia Baraza lako tukufu kuwa kuanzia tarehe 1 April mwaka 2016, serikali itaanza kulipa pencheni kwa wazee wote waliofikia umri wa miaka 70 *(universal pension)*. Hii Mhe. Spika, iwe umefanya kazi serikalini au hujafanya kazi serikalini, *as lounges* uwe umetimiza miaka 70, utapatiwa pencheni hiyo. Pencheni hiyo itatolewa kwa wazee waliofikisha umri huo bila ya kujali kipato chake na italipwa kwa kiwango cha TZS 20,000 kwa mwezi. Jumla ya TZS 1.65 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa ajili hiyo.

**Makundi Maalum**

Mhe. Spika, makundi haya yanajumuisha makundi yenye mahitaji maalumu kama vile watu wenye ulemavu, watu wanaoishi na UKIMWI na *VVU*, watumiaji wa dawa za kulevya na kadhalika. Kupitia sheria mbalimbali, serikali itaanzisha mifuko maalum ili kukidhi mahitaji ya fedha kwa makundi hayo na sehemu ya fedha za mfuko zitatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nimetumia muda mwingi kueleza mambo haya ili wananchi wenyewe waone vipi fedha zao wanazolipa kupitia kodi mbalimbali zinavyotumika. Aidha, imekuwa ni muhimu kueleza haya ili waweze kuelewa hatua zinazochukuliwa na serikali yao katika kutumia fedha chache zilizopo kutatua matatizo mbalimbali yanayowakabili. Nikizungumzia uchache wa fedha, naomba sasa nitoe uchambuzi wa Bajeti ya mwaka 2015/16.

**UCHAMBUZI WA BAJETI 2015/16**

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema, matarajio ya mapato ya ndani hadi kufikia mwezi Juni 2015 ni kufikia TZS 360.4 bilioni. Hatua za kuimarisha usimamizi wa mapato pamoja na hatua mpya zinazopendekezwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 zinatarajiwa kuongeza jumla ya TZS 90.1 bilioni na hivyo kufanya mapato ya ndani kufikia TZS 450.5 bilioni.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2015/16, matumizi ya lazima *(mandatory expenditure)* yatagharimu serikali jumla ya TZS 346.0 bilioni. Matumizi haya ni pamoja ni haya yafuatayo:

a) Mishahara ya Wizara na Taasisi zote zinazopokea ruzuku itafikia TZS 223.7 bilioni.

b) Matumizi ya kisheria ya Mfuko Mkuu wa Serikali (*CFS*) yamefikia TZS 53.4 bilioni ikijumuisha pencheni TZS 11.0 bilioni, Mishahara ya Mfuko Mkuu TZS 1.3 bilioni, malipo ya mikopo na riba TZS 20.95 bilioni na malipo ya viinua mgongo TZS 11.0 bilioni pamoja na malipo ya mafao ya wajumbe wastaafu wa Baraza la Wawakilishi na wanasiasa wengine ni TZS 8.5 bilioni.

c) Gharama za miradi yenye dhima *(Commited Projects)* TZS 39.1 bilioni, ikijumuisha kupandisha hadhi hospitali ya mnazi mmoja TZS 4.0 bilioni, ujenzi wa barabara Unguja na Pemba TZS 6.6 bilioni, ujenzi wa jengo jipya la abiria TZS 3.0 bilioni na uwekaji wa kamera na vifaa vya ulinzi TZS 10.0 bilioni.

d) Gharama za chakula cha wagonjwa ni TZS 0.3 bilioni.

e) Ruzuku za kisheria za TZS 29.5 bilioni ikiwemo, ZRB TZS 11.3 bilioni, madeski TZS 1.8 bilioni.

Matumizi haya ya lazima yatabakisha TZS 104.5 bilioni tu ya mapato ya ndani.

Mhe. Spika, pamoja na gharama hizo za lazima, serikali inakabiliwa na ongezeko la gharama mbali mbali zisizoepukika *(Committed Expenditure).* Matumizi hayo yasiyoepukika kwa mwaka huu, yataigharimu serikali jumla ya TZS 42.5 bilioni. Matumizi hayo ni pamoja na haya yafuatayo:

a) Gharama za uchaguzi mkuu TZS 7.5 bilioni.

b) Gharama zinazoambatana na awamu mpya ya serikali na Baraza la Wawakilishi TZS 1.8 bilioni.

c) TZS 1.65 bilioni zitatumika kwa ajili ya kulipia pencheni kwa wazee wote walio na umri kuanzia miaka sabini.

d) Gharama za huduma za afya ikiwemo ununuzi wa dawa na matibabu nje TZS 7.0 bilioni.

e) Uimarishaji wa huduma za elimu ikiwemo uamuzi wa serikali wa kutoa huduma zote za elimu ya msingi na mitihani ya elimu ya Sekondari bila ya malipo TZS 8.0 bilioni.

f) Ziada ya ruzuku ya pembejeo za kilimo ya TZS 500 milioni.

g) Malipo ya bili za umeme kwenye visima vya maji ni TZS 4.5 bilioni.

h) Baraza la mitihani TZS 2.0 bilioni.

i) Mkopo wa elimu ya juu TZS 9.5 bilioni.

Mhe. Spika, matumizi haya yatabakisha jumla ya TZS 62.0 bilioni. Hali hii, ikizingatiwa pia na kutokuwepo kwa misaada ya kibajeti (*GBS*) iliokuwa ikifikia wastani wa TZS 40 bilioni, itapelekea kupungua sana kwa bajeti ya matumizi ya kawaida kwa wizara na taasisi zote za serikali pamoja miradi ya maendeleo.

Hata hivyo TZS 2.8 bilioni zinatarajiwa kupatikana kutokana na msamaha wa madeni pamoja na mfuko wa wafadhili na kupelekea jumla ya bakaa ya TZS 64.9 bilioni. Miradi iliyobakia ya maendeleo inatarajiwa kutumia jumla ya TZS 12.8 bilioni ambayo itapunguza bakaa hadi kufikia TZS 52.0 bilioni. Gharama za matumizi ya kawaida (TZS 65.7 bilioni) na matumizi mengineyo ya Mfuko Mkuu wa Serikali (16.3 bilioni) yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 82.0 bilioni, na kupelekea nakisi ya TZS 30 bilioni. Inapendekezwa kukopa ndani ya nchi kiasi hicho cha TZS 30.0 bilioni na hivyo kuziba nakisi yote ya Bajeti.

Mhe. Spika, serikali imeandaa utaratibu madhubuti utakaohakikisha matumizi mazuri ya fedha za umma kwa taasisi zake. Utaratibu huu ni pamoja na matumizi ya mfumo mpya wa bajeti unaozingatia matokeo (PBB). Uwazi wa mfumo huo, utawawezesha Wajumbe wa Bazara lako tukufu kuhoji matokeo ya huduma mbali mbali zinazotolewa na programu kwa kuangalia viashiria vya huduma hizo.

## SURA YA BAJETI KWA MWAKA 2015/16

Mhe. Spika, kutokana na maelezo ya hapo juu, Bajeti ya mwaka 2015/16 inatarajiwa kuwa na mwelekeo ufuatao:

### Mapato:

Mhe. Spika, Bajeti ya mwaka 2015/16, inatarajiwa kuwa na mapato ya jumla ya TZS 830.4 bilioni zikihusisha mapato ya ndani ya TZS 450.5 bilioni na mikopo ya ndani ya TZS 30 bilioni. Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo ambazo ni TZS 347.1 bilioni na TZS 2.8 bilioni za Msamaha wa madeni na Mfuko wa Wafadhili. Kwa upande wa matumizi, kati ya TZS 830.4 bilioni zinazotarajiwa, matumizi kwa Kazi za Kawaida yanatarajiwa kufikia TZS 431.4 bilioni na yale ya kutekeleza mpango wa maendeleo ni TZS 399.0 bilioni.

Mhe. Spika, kwa kuwa mchango wa maendeleo ni TZS 98.2 bilioni tu zinazotarajiwa kupokelewa kama ruzuku na kwa kiasi kikubwa Bajeti ya mwaka

2015/16 inategemewa itokane na fedha zetu wenyewe, ama za makusanyo ya ndani au mikopo itakayolipwa baadaye. Kutokana na hali hiyo, kiwango cha utegemezi kinatarajiwa kushuka hadi kufikia asilimia 12.2 tu. Kwa sababu hii, na kwa sababu ya fedha nyingi zilizoelekezwa katika huduma mbalimbali zinazolenga masuala muhimu ya kijamii, nathubutu kutamka kuwa Bajeti ya mwaka 2015/16 ni Bajeti ya Jamii na Kujitegemea.

Mhe. Spika, mfumo wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2015/16 utakuwa kama unavyoonekana katika jadweli hapa chini.

**Chanzo:** Wizara ya Fedha.

**L. SHUKRANI**

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali, kikao hichi cha Bajeti kinahitimisha miaka mitano ya uongozi wa awamu hii. Mosi, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Nawashukuru kwa kutuamini na kuturuhusu kuwatumikia kwa kipindi chote cha miaka mitano, nawashukuru kwa imani yao muda wote wa kipindi hicho, na nawashukuru kwa utulivu wao mkubwa waliouonesha ambao umetusaidia sana katika kuwatumikia vyema.

Mhe. Spika, Pili, naomba pia kwa niaba ya Serikali kukushukuru sana wewe binafsi Mhe. Spika na Mhe. Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Zanzibar kwa uongozi wenu katika mihimili ya Baraza la Wawakilishi na Mahakama uliokuwa na mashirikiano makubwa na mhimili wa utawala wa serikali. Bila ya shaka, kupitia kwako Mhe. Spika, nawashukuru sana Mhe. Ali Abdulla Ali, Naibu Spika, na wenyeviti wote wa Baraza ambao wamekuwa wakikusaidia wewe unapodharurika. Mashirikiano yenu yametusaidia sote kuwa na utulivu wa kutekeleza majukumu yetu na kuwatumikia wananchi wenzetu.

Mhe. Spika, tatu naomba kuwashukuru sana Waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza hili kwa mashirikiano makubwa kwa kipindi chote cha utendaji wetu wa pamoja. Kwa namna maalum naomba pia kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la wawakilishi, Mhe. Hamza Hassan Juma, na wajumbe wake ambao ni, Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali (*PAC*), Mhe. Omar Ali Shehe Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, Mhe. Hija Hassan Hija, Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari Mhe. Mlinde Mabrouk Juma. Kwa nafasi yangu pia nimefanya kazi na kwa karibu zaidi na Kamati tatu; ya Wenyeviti wa Kamati za

Kudumu, Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Kati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Najihisi nina deni kubwa la kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati hizi kwa mashirikiano yao kwangu. Nasema Ahsanteni sana nyote.

Mhe. Spika, nne, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Makatibu Wakuu chini ya uongozi wa Dk. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Kiongozi, kwa ushauri wao ambao umekuwa chachu ya utendaji mzuri wa serikali yetu. Bila ya shaka, shukurani hizi zinawahusu pia watendaji wakuu na wafanyakazi wa wizara mbali mbali, idara zinazojitegemea, Mikoa, Wilaya, Baraza la Manispaa, Halmashauri za Wilaya, Mabaraza ya Miji, Asasi zisizo za Kiserikali pamoja na Sekta Binafsi. Wote hawa tumefanya nao kazi kwa karibu sana na tumenufaika sana na michango na kujitolea kwao kiutaalamu, kihali na mali.

Mhe. Spika, kazi yangu ya uwaziri imesaidiwa sana na utendaji makini wa wasaidizi wangu mahiri. Naomba niwashukuru kwa namna ya pekee kabisa ndugu yangu Khamis Mussa Omar, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Bi. Amina Khamis Shaaban, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango ambaye awali alikuwa sehemu ya iliyokuwa Ofisi ya Rais – Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo niliyokuwa nikiongoza hadi mwezi Agosti mwaka 2013 ambapo kazi za Mipango zilitenganishwa kimuundo na zile za Fedha. Namshukuru pia ndugu Juma Ameir Hafidh, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Omar Hassan Omar, Mhasibu Mkuu wa serikali, Ndugu Mwita Mgeni Mwita, Kamishna wa Bajeti, Makamishna wote, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Taasisi zake kwa utendaji wao katika kipindi chote cha miaka mitano inayokaribia kukamilika mwaka huu.

Mhe. Spika, kipindi cha miaka hiyo mitano tumefanya kazi kwa karibu na kunufaika na msaada na mashirikiano na nchi rafiki na Mashirika ya kimataifa. Kwa niaba ya Serikali, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Wananchi wote wa Zanzibar, naomba kuthamini na kushukuru sana mashirikiano na msaada wa nchi za Canada, China, Cuba, Denmark, Falme za Kiarabu, Finland, India, Ireland, Japani, Korea ya Kusini, Kuwait, Marekani, Misri, Norway, Oman, Saudi Arabia, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uturuki.

Mhe. Spika, kwa upande wa mashirika ya kimataifa, naomba nishukuru misaada ya: ACBF, ACCRA, AfDB, AGRA, BADEA, CARE INTERNATIONAL, CDC, CHAI, CIDA, DANIDA, DFID, EGH, EU, EXIM Bank ya China, EXIM Bank ya Korea, FAO, FHI, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, IAEA, ICAP, IDB, IFAD, ILO, IMF, IPEC, JICA, JSDF, KOICA, MCC, NORAD, OFID, ORIO-Netherlands, PRAP, SAUDI FUND, Save the Children, SIDA, UN AIDS, UN, UNDP, UNESCO, UNFPA, UN-HABITAT, UNICEF, UNIDO, USAID, WB, WHO na WSPA. (*Makofi*)

## HITIMISHO

Mhe. Spika, kwa kuwa tumekabiliwa na mchakato wa kidemokrasia unaowataka Wananchi kuchagua Viongozi wao wa kuwaongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, naomba nihitimishe kwa kuwaomba sana Viongozi wa vyama vya siasa, wanachama wao na wananchi kwa ujumla kuhakikisha kuwa tunatumia fursa yetu hiyo ya kuchagua viongozi wetu kwa amani, udugu na upendo mkubwa. Tunaweza kuchaguana bila ya kuumizana. Tunaweza kuchaguana bila ya kupigana. Tunaweza kuchaguana bila ya kuhasimiana. Kila mmoja wetu ana dhima ya kuhakikisha uchaguzi Mkuu wa mwaka huu unakuwa wa mfano kwa utulivu na mafanikio. Kila mmoja wetu autimize wajibu huo.

Niitumie pia fursa hii kuwatakia kheri Waheshimiwa Wawakilishi wote wanaokusudia kuomba tena ridhaa ya Wananchi kuwaongoza tena katika Majimbo yao. Tuelewe tu kuwa Wananchi ndio waamuzi, watakapochagua itakuwa ndio wamesema. Tuheshimu kauli yao na kuikubali bila ya kinyongo kwani sote ni Wazanzibari na Watanzania. Katika kutafuta ridhaa za wananchi lugha zetu zina nafasi kubwa. Wakati wa kampeni tutumie lugha ambazo zitajenga umoja wetu na kuifanya Zanzibar yetu iwe na Amani; bila ya Amani ule msemo wa "Zanzibar ni njema atakae aje" utakuwa hauna maana.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa kwa heshima na taadhima naliomba Baraza lako tukufu lipokee, lijadili na hatimaye kwa kauli moja liidhinishe makadirio ya mapato ya Shilingi milioni mia nane na thelathini bilioni na mia nne milioni (TZS 830.4 bilioni) na matumizi ya kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kugharamia kazi za kawaida za Shilingi milioni mia nne na thelathini na moja bilioni na mia nne (TZS 431.4 bilioni) na kwa upande wa Mpango wa Maendeleo kutumia Shilingi mia tatu na tisini na tisa bilioni (TZS 399.0 bilioni) kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunisikiliza na sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha hotuba hiyo ya bajeti ya mwaka 2015/2016 hotuba ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameunga mkono. Taratibu zinatutaka kwamba suala hili la Hotuba ya Bajeti pamoja na Hotuba ya Mpango wa Mendeleo iliyosomwa asubuhi vyote vije vijadiliwe kwa pamoja. Kwa hivyo niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kusikiliza kwa makini sana na pale ambapo kulikuwa kuna maneno ya msisitizo mmepiga makofi mengi kuonesha kuafiki mambo hayo.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea na hatua nyengine taratibu zinatutaka kwamba masuala haya yaje yajadiliwe hapo usoni kuanzia siku ya Jumatatu. Kwa hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) nataka nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi atoe hoja ili kuahirisha masual ya majadiliano mpaka siku ya Jumatatu kwa mujibu wa Kanuni hiyo.

## KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Kwa kuwa shughuli zilizo mbele yetu zimekamilika na kwa kuwa Mhe. Waziri wa Fedha amekamilisha Hotuba ya Bajeti na kwa kuwa tuna Hotuba ya Bajeti na hotuba ya Mpango wa Maendeleo, hivyo naomba Baraza lako Tukufu liahirishe kikao chake mpaka tarehe 18/05/2015 saa 3.00 asubuhi barabara ili tukutane tena na tuweze kujadili hotuba hizo zilizowasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi wale wanaokubaliana hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Kabla hatujaahirisha shughuli zetu za leo katika shughuli hii ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tumewaalika wageni mbali mbali na ninawashukuru wengi wao wamefika, kwa hivyo itabidi na ni utamaduni wetu kuwatambua wageni ambao tuliwaalika na wakabahatika kufika.

Kwa hivyo kwanza nitambue kuwepo kwake Mhe. Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninamuomba asimame. Tumemualika pia mama Asha Suleiman Idd mke wa Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi na yeye tumemualika na yupo. *(Makofi)*

Naomba nichukue nafasi hii na fursa hii and *I am very much delighted to recognize the Council General were present here in Zanzibar who are Council General of India may he rise up, if he is there; Council General of Msumbiji, if he is there; Council General of China, Council General of Oman, Council General of Egypt - Misri could he rise up if he is there, Ambassador of Sweden, is not there; Ambassador of Norway and Finland, they are Council General honorary, could they rise up if they are there to salute the members, they are not there. Council*

*General honorary of Germany, not present and Council General of Italy honorary, not present.*

Tunao vile vile wawakilishi wa mashirika ya kimataifa, *I have the pleasure to recognize all of them from UNDP, UNFPA, UNICEF WHO, IMF.* Naomba vile vile niwatambue kuwepo kwao Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu wa Wizara mbali mbali za SMZ, naomba wasimame kwa pamoja.

Nina furaha vile vile kutambua kuwepo kwa mke wa Spika na familia yake, namuomba asimame. *(Makofi)*

Katika mkutano huu tumewakaribisha vile vile Makamanda na Makamishna wa Vikosi vya Ulinzi vya SMT na SMZ naomba wasimame kwa pamoja. *(Makofi)*

Naomba wasimame kama wapo wawakilishi wa vyama vya siasa viliopo Zanzibar wale pale. *(Makofi)*

Naomba pia nitambue kuwepo kwake Msajili wa Vyama vya Siasa, inaonekana hajafika. Naomba niwatambue Wenyeviti wa Tume mbali mbali za Utumishi Zanzibar kama wapo kwa pamoja wasimame, hawapo. Naomba nitambue kuwepo kwa Mameneja na Wakurugenzi wa Taasisi mbali mbali za Serikali kama wapo naomba wasimame, wale pale. *(Makofi)*

Tuliwaalika pia Wakuu wa Vyuo Vikuu viliopo Zanzibar kutoka SUZA *Vice Chancellor* kama yupo, hayupo. Kutoka *Zanzibar University* Professor Roshashi, *Vice Chancellor* kama yupo, hakufika. *Vice Chancellor wa Abdulrahman Al-Sumait Memorial University* Chukwani kama yupo, yule pale. *(Makofi)*

Naomba nitambue vile vile Wakuu wa Vyombo vya Habari. Kwanza Mkurugenzi Mkuu wa *ZBC*, Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Mkurugenzi wa *Zanzibar Cable Television*, inaonekana hakufika.

Naomba niwatambue sana waandishi wote wa habari ambao kwa muda mrefu wanashirikiana na sisi, wengine ndio hao wanatuonesha katika *camera* zao. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tunao utamaduni baada ya shughuli zetu hizi kujumuika hapo nje ili kubadilishana maelezo juu ya hotuba hii lakini wakati huo huo tukiwa tunatafuna tafuna hapa na pale. Kwa hivyo naomba niwaalike wote hapo nje ili tuweze kubadilishana mawazo wakati huo huo tukipata viburudishaji mbali mbali.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, ninawashukuru sana wageni wetu mliohudhuria na pia tunawashukuru wale ambao hawakuweza kuhudhuria tunajua mualiko wetu umefika kwao na walikuwa na nia thabiti ya kuja kushirikiana na sisi.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo sasa ninaahirisha kikao hiki hadi siku ya Jumatatu tarehe 18/05/2015 saa 3.00 barabara za asubuhi.

*(Saa 11.30 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 18/05/2015 Saa 3.00 asubuhi)*